# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

## Verbatim Report of

# CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, TAVETA CONSTITUENCY, HELD AT CHALLA HIGH SCHOOL

# ON

# May 03, 2002

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, , TAVETA CONSTITUENCY HELD AT CHALLA HIGH SCHOOL ON M**

**2002.**

**Present:**

1. Prof. A. Idha Salim - 1st Vice Chairman
2. Mr. Domizano Ratanya - Commissioner

**Secretariat Staff In Attendance:**

1. Collins Mukewa - Program Officer
2. Fidelis Wangatta - Asst. Program Officer
3. Lucy Aketch - Sign Language Translator
4. Grace Gitu - Verbatim Recorder

**Othoniel Munene:** Waheshimiwa mliofika hapa, Commissioner wa Tume hii ya kurekebisha Katiba yetu ya Kenya, wananchi

wa sehemu hii ambao mmefika kwa saa hii nzuri, mimi nawasalimu nyote, hamujambo? Sasa tunataka tuanze shuguli hii na kwa kwanza, hapa mbele yenu kuna maCommissioner hawa wawili. Huyu ako upande wangu hapa, yeye anatoka sehemu za huko Meru mbalilakini yuko hapa kwa kazi hiyo kuwasaidia ili achukue maoni yenu. Na huyu mwingine anatoka huko Mombasa huko yaani mbali; ingawa si mbali sana kuliko Meru, lakini yuko hapa kwa shuguli hiyo hiyo.

Na hapa pia kuna wale wanachama wa ile kamati iliyokuwa ikizunguka kuwaelezea jinsi ya kutoa maoni yenu. Wako hapa mbele yenu, wengine wako pale nyuma, kuna yule mama yule anaitwa Judith, tena kuna yule bwana mwenye kofia nyeupe kule, yeye ni wakamati ya……..na yule mwingine kule nyuma anasimamia upande wa vijana mambo ya vijana yeye ni na mwingine pia tulikuwa naye nafikiri ametoka kidogo hapa. Na mimi pia, na yule mama ako kule nje Dorothy, wote hawa munawafahamu kwa maana wamewazungukia sana.

Sasa kabla hatujaanza mambo haya naomba kwanza tujikabidhi wenyewe na kazi hii, kwa Mwenyezi Mungu. Ningemuomba bwana Ibrahim pale nyuma atusaidie kwa maombi.

**Ibrahim Chapcha:** Nina wasalimu, habari ya asubuhi, mmeamuka aje wazee? Tuombe.

**Prayer:** Baba katika jina la Yesu Kristo, Mungu wetu, Mungu uishiye milele tunakuja mbele zako Mungu Baba asubuhi ya leo, tukisema ni asante mwokozi kwa mema yote umetutendea Bwana. Angalia Mungu umelinda wapendwa wetu ndugu zetu kutoka mbali, wamekuja hapa kwa ajili Bwana ya kuweza kurekebisha Katiba. Mungu wetu mambo haya yote Baba tunaomba Mungu wetu uwe pamoja nasi Bwana tunapoenda kuaanza kazi hii Baba; unajua kazi hii ni ngumu lakini Mungu wetu ukiwa pamoja nasi itakuwa rahisi. Tusaidie Mungu wetu, tunakataa hila zote za mwovu.shetani na mipango zake ambazo Bwana, mara nyingi huvuruga amani. Mungu wetu tunaomba Bwana ukatutetee ukatutangulie ili Bwana kila jambo lolote itakaloendelea mahali hapa, ikawa Bwana ni sawa sawa na mapenzi yako. Bwana tusaidie, anza pamjoa nasi Bwana hata ukimaliza pamoja nasi Bwana tutakushukuru. Tunaomba Bwana tukijua umetusikia mwokozi. Na yote tumeomba katika jina la Yesu Kristo ahye na mwokozi wa maisha yetu, Amen.

**Othoniel Munene:** Haya. Mutajiandikisha majina kule, wakati ya kuanza tutaanza na yule amejiandikisha kwanza halafu wa pili na kuendelea. Ukiwa ndani ya hii hall, hii sheria .ile ambayo inafanya kazi hii iendelee, inakupa ulinzi wa kutosha. Usiogope kueleza maoni yako ukifikiri "oh naweza kutaja hapa nikashtakiwa", hapana. Hata kama unona Rais anafanya hivi na hivi na unataka Katiba hii irekebishe sema. Hakuna mtu atakupeleka kortin ukisemea hapa ndani. Kwa hivyo musiwe na wasiwasi. Na wakati mtu anatoa maoni yake ni kwanza atoe yachukulwe na wewe muingine umeketi hukoo ikiwa mwenzako amesema jambo amblo wewe unaona si sawa kwako, hapana kumupigia kelele wala kumuambia "hapana" wewe utangoj nafasi yako na wewe useme yako. Wacha aeleze mambo yake halafu yataandikwa kila mtu mambo yake. Yule ambaye ameandika tayari anaweza kuja, atapewa dakika zake kidogo, kama anataka kuyasibiya kwa ufupi atasoma halafu atayapeana.

Kama anataka kupeana hiyo bila kuisoma maana ameshandika, inakubaliwa. Kama hukuandika unataka kueleza, utaeleza kama umekaa hapo unaeleza mambo yako yote. Kwa hivyo hakuna shida, usiwe na wasiwasi, mambo yako yatachukiliwa vizuri sana. Kwa hayo machache ningerudisha ushukani kwa maCommissioner wetu ili waendeshe jambo hili. Asanteni sana, nimesau kuwambia majina yao. Huyu bwana anaitwa Ratanya yule anayetoka Meru. Yule mwingine ni Professor Idha Salim kutoka upande wa Mombasa. Mimi munanifahamu naitwa Othoniel John Munene mwenyekiti wa hii kamati, iliokuwa ikishugulikia mambo haya.

**Com. Ratanya:** Sasa bila kupoteza wakati, kwa hayo mumeambiwa na bwana Chairman, sina mengi ya kuongeza isipokua tu niwajulishe ule mpango tutakokuwa nao kutoa maoni.

Kwanza kama vile umesikia, kama umeandika-hii tunaita memorandum unandika maoni yako hapo, unaweza kuja upeane pale na ikiwa hutaki kuongea chochote upeane, halafu uende ama uketi usikilize wengine. Ama kama unataka kueleza machache kwa yale ambayo umeandika utapewa dakika tatu, utapewa dakika mbili hapo kueleza yale machache ambayo umesema kwa hiyo memorandum. Na tena hata ingawa hujaandika na hayo maneno yatoka kwa mdomo wako, hujaandika pahali popote, ni maoni yako, utapewa dakika tatu uketi hapo na ueleze maoni yako kwa hizo dakika tatu. Kwa hivyo ikiwa umeandika, utapewa dakika mbili kwa kueleza machachama upeane hata bila kusema, hutalazimishwa kuongea kama hutaki. Lakini kama unataka kuongea, kueleza machache utapewa dakika mbili.

Na ukitaka kuongea bila kuandika utapewa dakika tatu. Na kwa kuzungumza utakuwa unaketi hapo utakuwa na microphone-sijui kama microphone iko hapo, itakuwa hapo na yale yote ambayo utasema, yatanaswa katika hii recorder yetu. Hiyo ni kumahanisha wakati unamaliza kupeana mambo yako, tutachukua kwa ule mtambo na kuenda nayo Nairobi pamoja na maandishi yako. Hata baadaye ukitaka kujua ulisema namna gani, hata hiyo nafasi pengine utapewakama ukishuku ukisema ya kwamba hukusema hivyo, utajisikia hapo kwa hiyo machine, hiyo tape recorder. Kwa hivyo wananchi ningetaka tuaanze sasa, na useme mambo yako kwa uchache usiwe unarudia yale yamesemwa na wengine sana kwa sababu tunataka kuwa na nafasi ya kuenda nyumbani mapema jioni. Hata nyinyi najua munatoka mbali na tungetaka kumaliza mapema jioni na ningetaka tuaanze na wa kwanza hapa anaitwa James Waweru.

**James Waweru:** Mimi sikuweza kuandika na nita ongea mambo mawili. Jina langu ni James Waweru, mukaaji wa……….location nimekaa hapo kwa muda wa miaka ishirini na tano.

Jambo langu la kwanza ningeanza nalo ni jambo la Wabunge. Ingekuwa ni jambo la muhimu sana ya kwamba kama Wabunge, kabla hawajajiongeza mishahara yao, wangekuwa wanarudi kwa wananchi. Napenda kusisitiza kwamba wakati Wabunge wanajiongezea half a million wakati hospitali zetu hata asprin hakuna, wakati wananchi wa kawaida wanashindwa kununua chumvi hata ya shilingi tano, jambo hilo linaonyesha ya kwamba Wabunge wetu hawafikirii maana ya wananchi.

La pili na ni hilo, hilo; imestahili wananchi wapewe uwezo wa kukataa mjumbe au kumurudisha wakati wanaona ya kwamba mambo hayaendi sawa sawa kwa upande wa uongozi wake. Nikitoka hapo kwa sababu dakika nime ambiwa ni kidogo, ningeomba ya kwamba Kenya yetu vile iliviyo ni nchi ndogo na ni nchi ambayo haina mali nyingi, ni nchi ambayo ina umaskini mwingi huwezi kuilinganisha na nchi zingine za dunia. Ingestahili iwe ni Kenya moja, yenye serikali moja na serikali ya mitaa ziwe na uwezo-I mean Local government ziwe na uwezo. Sababu ya kusema hivyo ni kuonyesha kwamba Kenya tuko makabila zaidi ya arubaini na kama ikigawanywa nusu nusu, ukabila utakuwa wa hali ya juu sana katika Kenya na ukabila ndiyo adui ya maendeleo katika nchi yeyote ile. Kwa hivyo maoni yangu ni kwamba Kenya iwe Kenya moja na Kenya ambayo makabila yanaishi kwa umoja na kwa heshima, na kila kabila hata kama liko mahali gani, linakuwa na uwezo kuwaheshimu kabila ile iliokuta. Ukiwa uko Maasaini unaheshimu Maasai, ukiwa uko Nandi muheshimu Nandi, ukiwa uko Embu muheshimu Embu, ukiwa uko Ndia muheshimu muishi kwa…….moja na hiyo ndiyo kujenga Kenya moja. Asante sana.

**Com. Ratanya:** Okay. Asante sana Bwana Waweru, na Waweru uende pale. Waweru, hebu keti hapo, utapata swali moja kutoka kwetu.

**Com. Prof. Idha Salim:** Mzee Waweru labda ungenieleza kidogo wazi wazi, hasa ungependelea jambo gani lifanywe kuhusu Wabunge? Umesema kwamba wanapata mishahara mikubwa na hali wananchi hawana hata pesa ya kununua chumvi. Ungependelea ifanywe kitu gani?

**James Waweru:** Ningependelea wakati kuna jambo hawa wanataka kujiongezea mishahara, irudi kwa wananchi, maana wananchi ndio the stakeholders they are tax payers.

**Com. Ratanya:** Okay, asante Bwana James Waweru kwa hayo maoni yako, na sasa tungetaka kuenda kwa Ibrahim Mukeremu.

**Ibrahim Chapcha:** Mimi na shukuru kwa sababu mimi ni Ibrahim Chapcha na maoni mengi tumeandika kwa pamoja lakini nataka tu niseme maneno mawili, matatu.

Ni kwamba wakati mwingi tunapokuwa katika hali tuseme ya-nilikuwa nasema tu kwamba wakati-yaani jambo ambalo ninaona la muhimu sana kwa serikali yetu ukiangalia wakati ule kwa mfano tunapoenda kuchagua, labda tunaweza sema tunachagua Mbunge tungetakikana, katika maoni yangu, ningeona kwamba kuna umuhimu wa kuangalia kwamba, yaani mara nyingi tunapochagua Mbunge tunashindwa kuchagua, labda unakuta pengine tuko wachache. Labda wale wenyeji wangepewa ile nafasi ya kwanza.

Kwa mfano inaweza kuwa kwamba ni Wabunge wanachaguliwa, unakuta tu mtu anakuja labda ametoka mbali, si mwenyeji lakini amekuja tu kwa kutafuta kile kiti. Hajui mawazo, hajui ile shida ya ile sehemu. Sasa utakuta katika ile hali inakuwa watu

hawasaidiki kwa sababu yule mtu amekuja tu na kupata kwa hila tu labda kwa kujinufahisha kibanafsi . Lakini ingekuwa kwamba mwenyeji angepata, angekaa pale, ni mtu ambaye atajua eneo hilo na shida za wale watu walioko pale. Kwa hivyo unaweza kusaidika vizuri zaidi.

Najua ni mengi ambayo tayari tumeandika kwa pamoja lakini nilikuwa tu nasema kwa maoni yangu kwamba, kama inawezekana basi, kwa sababu unakuta sehemu zingine wale wenyeji unakauta labda ni wapungufu, hawatoshi. Lakini sasa kutokana na ile hali ya kwamba ule mlolongo, basi inakuwa kwamba yule anachaguliwa pale anaingia tu kwa sababu ya kibinafisi, Lakini ningeomba kwamba kama inawezekana, wale Wabunge wanapenda kuchaguliwa, serikali yetu pia iangalie vile wale wenyeji wa ile sehemu.

Lile lingine nilikuwa nasema ni kwa upande wa ardhi. Wale wenyeji wa ile sehemu wapate nafasi ya kwanza katika kugawanya ile sehemu: Unakuta wakati mwingine kunapogawanywa ardhi, wale wenyeji ambao wamekaa huko kwa muda mrefu, unakuta hawapati – ni wageni ndio wanapata nafasi hiyo. Ingekuwa vizuri kama wenyeji wangepewa nafasi ya kwanza.

Kwa hivyo nilikuwa naomba tu kwamba kama inawezekana serikali yetu iangilie hayo mambo mawili, matatu. Hayo mengine yote tumesha rekebisha kwa pamoja; lakini hayo ni yale ambayo nilikuwa naona kwamba kama kunawezekana, kuyatia nguvu yale ambayo tunaweza kuyaandika.

**Com. Domizano Ratanya:** Bwana Ibrahim, unajua kikao hiki ni cha Tume ya Kurekebisha Katiba. Hiki si kikao cha serikali yenyewe huko; ni kikao cha kurekebisha Katiba ambako tunanasa maoni yenu, pia itusaidie kurekebisha hii Katiba yetu. Kwa hivyo ungependekeza nini-maoni yako, kusaidia hii Tume kurekebisha Katiba?

**Ibrahim Chapcha:** Ndiyo maana nimesema ya kwamba, katika maoni yangu vile ambavyo nilivyona, yaani katika kurekebisha Katiba, sasa serikali ile mpya ambayo itaenda kuwa, katika Katiba hii mpya, kuwe kuna umuhimu wa kuangalia mwenyeji kupewa ule mstari wa kwanza. Sio mtu tu anaweza kutoka pale, wengine wametoka Machakos ama labda wametoka kwa mfano sehemu mbali anakuja tu tayari na kuingia katika Ubunge na kuchukua kile kiti- hajui wenyeji ya wakoje. Lakini kwa sababu ana pesa, ame honga honga pesa, sasa anasimamiwa na wale watu, amepata wafuazi wa kumufuata. Sasa kwa sababu ya ule mlolongo, inabidi achukue kile kiti-kwa sababu ana pesa zake, ama ana uwezo kwa hali yote lakini nafasi hiyo ingefaa ipewe wale wenyeji. Halafu hawa nao ikija kwa wageni basi iwe kwanza yule mwenyeji apate ile kwa sababu inapokuwa mtu ambaye humjui na yeye hakujui, hawezi kukusaidia chochote.

Lakini kama amekuwa mtu ambaye ametoka pale pale, basi atajua shida yako, na yale matatizo yako na hali ya pale mahali; kama ni barabara, kama ni nini, kama ni mashamba-kila kitu anajua wewe ukiwa na shida haina yeyote.

**Com. Ratanya:** Point yako tumepata-ilikuwa kidogo tu, kueleza kidogo. Okay sasa uende pale. Na sasa tutaenda kwa

Nguso Karitie.

**Nguso Karitie:** Ninashukuru sana kwa ajili ya Katiba hii. Tungeliomba serikali yetu-ile iliyoka na ile itakayokuja kuwa ishuguhlikie jambo la sehemu ya wanyama pori na pale wananchi wanapoishi. Tumefungiwa sana na wanyama pori kwani wamechukua sehemu kubwa kuliko ile mwananchi anaishi.

Wanyama hao wanazurura-zurura kila pahali. Binadamu wa kawadia hawawezi kutembea maili nne kwa hali ya wanyama; lakini mnyama yule anaruhusiwa na serikali atembee popote kusumbua mwananchi wa kawaida, kuharibu chakula ya mwanachi wa kawaida. Pia nirudie mara ya pili, katika ardhi na ziwachiwe wakaaji kumiliki ardhi na makao.

Ya tatu, Misitu ya wananchi wa kawaida, serikali iangalie, wahudumu jinsi wanavyokaa kwa makao yao. Sina mengi kwa hivyo ninawachia hapo kwa haya Marekebisho ya Katiba ya Kenya.

**Com. Prof. Idha Salim:** Okay. Mzee Nguso ungenieleza kidogo kiwazi-wazi hasa ungependa maeneo hayo ambapo kuna wanyama yafanywe nini, yapunguzwe?

**Nguso Karitie:** (inaudible)

**Com. Ratanya:** Okay. Asante Bwana Nguso. Sasa tuende kwa Patrick Murisha.

**Patrick Murisha:** Kwa majina naitwa Patrick Murisha, ningekuwa napanda miti hapa tangu(inaudible). Kwanza ni eneo la Council ama ward ya Chala ni kwamba wadi hii, katika electoral system and process katika specified demarcation of Constituencies. Sehemu hii ni kwamba ni ward lakini ni kubwa sawa sawa Constituency. Ni kwamba Councillor ama diwani anaye wakilisha sehemu hiyo, hawezi kutoa huduma sawa ama inavohitajika. Ni sehemu ambao ina idadi ya watu wengi, na kwa kweli ilikuwa inalstahili igawanywe.

Pia kuna mambo ya operations za Local councils. Tungependa kuwa, Central Government isiwe inaoperate ama ku-govern hizi Local Authorities ama hizi Councils zetu. Kwani kiasi kile ambacho hupatikana katika hizi Councils zetu, pesa nyingi sana ikienda huko ni kama yote inabaki huko na sisi hapa tuna matatizo. Kwa hivyo tulikuwa tunataka kama pesa zile ndogo zinazopatikana katika Councils zetu, hizo pesa zibaki hapa na watu wenyewe wajipangilie vile zitakavyo saidia kwa maendeleo yao.

Nilikuwa na kitu cha mwisho kuhusu rasilmali. Ni kwamba mojawapo ya rasilmali-katika kitengo cha rasilma zile rasilmali zinazopatikana katika hiyo sehemu, kwa mfano hapa Taita Taveta ziweze kufaidi watu moja kwa moja; kwa mfano mapato ya

mbuga za wanyama. Tungeomba kitengo fulani-certain portion inafaidi locals wa hapa na ijulikane ni kiasi fulani, kiasi gani. Sina mengi kwa hayo.

**Com. Ratanya:** Okay. Asante sana Bwana Patrick Murisha na sasa tutaenda kwa Lesbulu Mushigati.

**Lesabulu Mushigati:** Thank you Commissioners. My names are Laban Lesabulu Mushigati, I am a teacher and I am presenting to you the opinions that were discussed by the teachers in Taveta Division. I wish to bring to you as follows.

Preamble. The Constitution of Kenya should have a vision on good governance and principles of state policies. Two; The Constitution that contains laws governing everybody- it should not be for the poor or for the rich. Directive Principles of state policy;

**Com. Ratanya:** Na kama una memorandum Mr. Lesabulu tuambie kwa machache yale yako hapo halafu utupatie memorandum.

**Lesabulu Mushigati:** Asante. Okay, we went through these items and we discussed on directive principles and state policy, Constitution supremacy where we say the public should be involved in Constitution amendments on 50% votes. And on citizenship, we said that a citizen of Kenya to be regarded as automatic one should be that one who has attained the citizenship by birth or naturalization.

On political parties, we suggested to the Commission especially in this Constitutional Review Committee to have only three political parties in Kenya and each political party should be made up of 28% of the total population of Kenyan voters. Structure and System of Governance; We said and we suggested to the Constitutional Review Commission, that the presidential system of governance should be retained. The Legislature; We agreed that we present this as; Contestants should have acquired a minimum pass in O Levels and above and this should be from the indigenous citizens. The Executive; The Constitution should set limits on the Presidential powers-one being above the law, the appointment of Vice Presidents and other government officials. And the Local government, we said that Councils should not continue to operate under the Central government and that they should be independent. Thank you.

Management and use of natural resources. We also have environment and natural resources and succession and transfer of power. In this we said during Presidential elections, the Permanent Secretary in the Office of the President should be the executive in charge. Thank you for that much.

**Com. Ratanya:** Okay. Thank you very much Mr. Lesabulu. Now we go to the next one. Mwingine ni Margaret Leshamta.

**Margaret Leshamta: Translation:** Jina ni Margaret Leshamta. Mama anasema, hapa Taveta anaona mambo hayaendi sawa sawa; Hata kwa upande wa mahospital, ukienda pale hakuna dawa hakuna chochote, mpaka ukanunue. Anasema upande wa urekebishaji wa mabarabara haoni kama unafanyika sawa sawa hata kama watu wakipewa ile tender ya kutengeneza barabara, wanaweka viraka-viraka tu na njia haipitiki. Ninatoa asante kwa hayo machache sina zaidi, hayo yanatosha.

**Com. Prof. Idha Salim:** Asante mama kwa maoni yako. Kuhusu huduma za kidawa ungependelea tufanye kitu gani?

**Margaret Lashamta: Translation:** Mama anasema, anaomba kwamba dawa zipatikane na ziwe ni bure na madaktari waletwe mpaka vijijini.

**Com. Ratanya:** Asante sana Margaret. Sasa tutaendelea kwa mwingine anayefuata ni Sisi Leshalta.

**Sisi Leshalta: Translation:** Jina yangu ni Sisi Leshalta. Nafurahi kwa mpango huu wa kurekebisha Katiba ya kutusaidia katika nchi yetu. Shida ilioko hapa Taveta kwetu, ni njia- communication. Njia hakuna za kutusaidia kuenda mashambani na kuenda popote pale. Mvua ikinyesha hakuna namna yoyote ya usafiri.

Shida ya pili, usambazaji wa umeme kwenye vijiji. Taveta hii hakuna, iko kwa sehemu ndogo sana. Naomba hiyo itiliwe maanani. Ingine sijui kama nitamwinglia mzee Waweru, ni hii mambo ya Wabunge kuongeza mshahara wao wenyewe, na mwananchi wa kawaida hana chochote, hata pesa ya kupeleka mtoto hospitalini. Angalao wangefuta hiyo pesa tunayotoa katika hospitali-hospital iwe ya bure kama zamani hapo ingekuwa sawa. Lakini sasa Wabunge wamejiongeza mshahara wenyewe hata madaktari wanashindwa hata kununua madawa. Yangu ni hayo.

**Com. Ratanya:** Asante Mama. Okay Chairman ningetaka afafanue kitu kimoja. Hapa umesema kuwa hamuna kama communication-ni kama Radio ama kama T.V.? Kwanza alisema Roads, lakini kuna mawasiliano mengine. Umeme-okay simu. Okay asante sana tumeipata. Sasa tuende kwa Nahuru Nyatia.

**Nahuru Nyatia:** Kwa majina naitwa NahuruNyatia. Maoni yangu ni matatu tu, sina lingine la kuongezea.

Oni la kwanza. Tunaomba kuhusu Katiba hii ya leo, kwamba watoto urithi kwa mji uwe sawa katika watoto wa kiume na wa kike. Lingine, kuhusu mtoto wa miaka kumi na nne aki bakwa, huyo mtu afungwe miaka ishirini-kwa sababu awe na ugonjwa, asiwe na ugonjwa asha potezea mtoto maisha yake.

La tatu. Tunaomba katika Katiba hii ya leo, mpange walimu wananyanyasika sana katika mambo ya mshahara. Wao ndio wako kiwango cha chini, tunaomba mtekeleze hilo jambo sababu bila mwalimu, hakuna maendelo duniani popote pale. Yangu

ni hayo tu.

**Com. Ratanya:** Okay asante sana kwa hayo maoni yako Nahuru, kwa hivyo tutaenda kwa mwingine this is Mrs. Kenu Lekilanu. Kwa hivyo huyu ameleta maandishi yake tutaenda kwa mwingine, Judith Leshamta.

**Judith Leshampta**: Maoni yangu juu ya Katiba. Jina langu ni Judith Leonard Leshampta. Namba ya kitambulisho ni hiyo 0661489.

Kanuni ya kuongoza sera za Dola; Ni lazima maadili yawe yakutekeleza kisheria. Ukuu wa Katiba; Wananchi wahusike kupitia mikutano ya maoni katika kubadilisha Katiba zile ambazo zinafinya wananchi wa kawaida. Mikutano hiyo iongozwe na Tume ambayo imeteuliwa ya marekebisho ya Katiba. Uraia; Atakaye pewa uraia bila swali, ni yule ambaye ana cheti cha kuzaliwa na cheti cha ndoa na wazazi wake ni wa mahali pale. Mtoto aliyezaliwa na mzazi mwana mume wa Kenya ambaye anacheti cha ndoa apewe uraia.

Vyama vya kisisasa; Kuwe na idadi maalum ya kyama vya kisiasa-viwe tu viwili. Muundo na aina za serikali; Tuwe na muuondo wa serikali ya majimbo ambapo mamlaka ya nchi na Bunge yame gawanywa baina ya serikali kuu na majimbo na pia ni mipaka iheshimiwe. Kazi ya Mbunge; Kazi ya Mbunge iwe kila siku. Mamlaka ya nchi; Katiba itoe kibali ili Rais aweze kuondolewa mamlakani kwa kitendo kisicho halali. Rais awe Mbunge wa jamii aliotoka. Serikali za mitaa; Mayor na mwenyekiti wa baraza wachaguliwe na watu au wananchi. Wananchi wawe na haki kurejesha nyumbani diwani au Mbunge wao. Madiwani wa ku tueliwa wateuliwe na watu kwa kupiga kura. Muundo wa uchaguzi; Tutafute muundo wa kura ya siri, na aliye pata kura zaidi ndiye mshindi. Tuwe na utaratibu wa kura za siri na tubadilishe utaratibu wa kura za mlolongo mwaka huu wa elfu mbili na mbili. Haki za kimusingi; masharti kuhusu kiKatiba ya kimsingi haitoshi. Haki za jamii kiuchumi, kiafya, kielimu, utamaduni---(interjection)

Sasa, haki za makundi yanayo weza kudhuriwa; haki za wanawake zipewe kikao mbele maana wame udhurika miaka mingi. Haki za ardhi; jamii mahali pale, inafaa imiliki ardhi ya mahali pale. Haki ya wanajamii tafauti za kitamaduni na kikabila. Mimi ndio mimi najichukulia kwamba ni mtu wa kikundi maalum cha jamii ambacho masilahi yangu yanapaswa kulindwa na Katiba.

Divorce; Mali yote tuliochuma na yule mume igawanywe sawa. Mali ya family, yaani family property; Majina ya bibi na bwana yaandikwe yote pamoja katika mali ile yote. Maternity leave; Maternity leave iwe miezi mitatu bila kufanya kazi. Domestic violence; Serikali ichukue hatua kwa baba aliempiga bibi yake. Walemavu; Walemavu waangaliwe maana hawakupenda kuwa hivyo. Ulawiti, ama sodomy; Mtu atakaye mlawiti mtoto chini ya miaka kumi na nne afungwe maisha-miaka kumi na tano kuenda juu; afungwe miaka kumi na tano kuenda juu. Mbuga za wanyama wa pori; Ranch ziwe game reserve ili wananchi wafaidike. Ikiwa haitawezekana, asilimia arubaini ingie kwa wilaya----(inaudible).

Maji-ambayo ndio ya mwisho; Wenyeji wa jamii wapate maji bure au kwa malipo kidogo wasifananishwe na watu wa miji ya mbali kama Mombasa, Nairobi na Kisumu. Asante kwa hayo machache.

**Com. Ratanya:** Okay. Asante sana Judith, sasa tutaendelea kwa anayefuata, ambaye ni Sophie Munene. Sophie Munene. Haya, amepeana Mandishi yake, sasa tuende kwa Francis C. Kimboi.

**Francis Kimboi:** Asante. Nina swali moja tu kuhusu-kwa jina naitwa Francis C. Kimboi. Nina swali moja tu ya kuhusu Njama. Naomba Katiba ipatie Njama nguvu za kutosha kama zamani. Maana Njama ndiyo ilikuwa serikali yetu kuu ya………. Asante.

**Jumanne Saleh:** Kwanza ningetaka kwa sababu watu wengi wa sehemu hii ni wakulima- Jina ni Jumanne Saleh. Ya kwangu ningetaka kwa sababu sehemu hii watu wengi ni wakulima, zaidi wao wanangaliwa haki zao haswa kwa masoko, kwa sababu masoko wanaopeleka si mazuri-kwa sababu wakienda pale hawapati chochote. Sasa wakiangiliwa kwa vizuri, kwa sababu wengi hapa ni wakulima, ingekuwa bora zaidi na umaskini ungepungua sana.

Iingine ni upande wa elimu. Ningetaka hiki kiti kitiliwe maanani kwa sababu kuna watoto wengi wako manyumbani hawaendi shule. Itiliwe maanani watoto hawa wapate elimu, kata wazazi wao ifulikane ni shida gani ili wapeleke watoto shule. Ingine ni upande wa secondary, (inaudible)iteremshwe kwa sabubu wazazi wengi wanashindwa kuelimisha watoto. Yangu ilikuwa ni hayo mawaili.

**Com. Ratanya:** Asante sana Bwana Jumanne na tuende kwa mwingine ambaye ni Thomas J. Nguzo.

**Thomas J. Nguzo:** Asante sana. Kwa majina najulikana kama Thomas Jumanne Nguzo. Nafikiri mimi nimekuja na memorandum (inaudible)lakini nina machache pia ya kuongezea, na haya ni kama ya futayo.

Nigependa Katiba ya itilie maana ni kwanza upande wa Wabunge. Mbunge anapochaguliwa kitu cha kwanza, awe mwenyeji asili wa sehemu ilie; kwani watu huwa wanakimbilia hicho cheo na sababu kubwa inakuwa ni ule mshahara wanaangalia pale lakini hawajui matatizo ya wenyeji ni vipi. Vile vile inatakikana huyo Mbunge pia, si ati apitishwe au amepita kwa kura mbili peke yake anachukuliwa kama Mbunge; inatakikana awe na percentage-iwe ni over 50% of the population. Awe amepitishwa na wengi. Mara utakuta Wabunge wengine wamechaguliwa na wachache, inakuwa wengi wa pale hawa mpendi. Yuko pale lakini hapendwi na wengi-lakini inasemekana amepita. Intakikana at least kama ni runner-up pia kama itakuwa ile kiwango haijatoshea. Wale runners-up warudi tena uwanjani wa-compete hicho kiti ilo at least wengi wawe ndio walimpitisha-isiwe ni wachache.

Jambo la pili, ningetaka kuongea about game reserves-hizi game parks, national game parks. Kwa kweli hapa Taveta, ni kama

sisi ni kama tunagandamizwa sana na hawa wanyama wa pori. Wametulalia, na serikali na Katiba ili iliyoko ni kwamba inajali wanyama kushinda binadamu-maana kwa kweli huwa tunapitwa tukiambiwa ukiguza tu-huyu mnyama anaitwa ndovu, ukimuguza tu, ndege watashuka hapa kama nyuki. Na kwa kweli huwa tunapita hapa kuwachunga tu kama mbuzi. Wanapo tuingilia kutuharibia mimea wetu huwa tunatakaa tu kuwafukuza tu, na ni hatari kwetu sisi.

Kwa hayo hata ningeomba kwanza iwe katika Katiba ni kwamba, huyo munyoma wanaohusika na wanyama pori, wawalinde wakae mbuganihuko. Otherwise wakipita pia na sisi tuwe na kuru wakitukanyangia pia na sisi tukae sambomba na wao. Maana nafikiri Katiba inawaruhusu wao, tukikutwa huko kwa misitu zao huko pia tuna adhibiwa vilivyo. Pia sisi wakinigia tuwadhisu vilivyo.

Jambo lingine ni kuhusu squatter issue. Hii mambo ya squatter issue huwa ninaona kama Katiba ya wakati huu haisingatii sana maana mimi ninavyoelewa ni kwamba squatter anatakikana awe mwenyeji-lakini hapa utakuta squatter ni mtu mja-na sijui huyo squatter mja-kuja anatokea wapi hapo tangu sijui----akiota kama ndege. Nafikiri kuna mahali alikuwepo, kwa hivyo awe squatter mahali pake pa kuzaliwa-asiwe squatter mahali ya nchi ya mwingine- sehemu ya mwingine. Maana tayari ile ardhi labda ilikuwa budgeted na wenyewe halafu unakuta mwengine ametoka huko sijui ni mwizi, sijui ni nini, amekuja amekaa mahali kama hapa Taveta, imekuwa ni dumping place ya watu waovu wote.

Kwa hivyo tunataka kama ni squatter pia iwe at least Katiba inafuatilia na serikali inafuatilia kwamba huyu squatter alitoka wapi, alianzia wapi, kitambo aitwe sqatter mahali fulani. Na mambo ya settlement scheme. Settlement scheme nafikiri ikitolewa kama imetolewa tuseme mahali kama hapa Taveta, ina-settle wale watu wenyeji wa pale-at least kama kweli shida itakuwa imezidi nchini, at least inatakana at least 5% ndio wale wengine wangaliwe masilai yao lakini 95% iwe ni ku-settle wale watu wa pale pale, wenyeji wa ile sehemu.

Jambo lingine pia ningetaka kuongezea ni kuhusu mambo ya land. Unajua kama hapa tuseme hapa Taveta zamani tulikuwa tunajua kuna hawa local elders ambao walikuwa wamebansilia ratiba za ardhi. Lakini nafikiri ilivurugwa na serikali na pia haya mambo ya uongozi kuja- watu kuja kulet uongozi tofauti hapa-kuja kupigania viti hapa. Lakini tunataka kabisa Katiba izingatie hawa local elders wapewe nguvu kamili; Kama hapa kwetu tuna local elders ambao tunaita Njama. Wale ndio wazee waliokuwa wanatuongoza na kutuelekeza jinsi watu wanakaa na mipangilio-everything kufuatana na serikali. Kwa hivyo tunataka hawa local elders, Njama hiyo itpewe nguvu na Katiba ya leo. Basi hapo tutajua kweli mambo yetu yatakuwa sawa.

Upande ya education, kuna mambo ya education. Unaona kwa kweli serikali upande mwingine tunavyosikia, kama viongozi wanaayongea kwamba wanajali watu ambao hawajiwezi, lakini naona sio hivyo, kwani inatakikana kama kweli-kuna watu masikini kwa kweli na wanashindua kufundisha watoto wao, lakini sasa unakuta hata zile bursaries zinazotolewa, zinalenga wale watu ambao wanajiweza tayari. Kwa hivyo, at least hii ingepita kwa mashule, kama ni secondary schools, ipite through the Headmasters waangalie nani ana shida kubwa. Hiyo bursary iwe inalipwa kutoka pale pale shuleni. Iposiwe pale, unangalia ile

list, wanaangalia majina, nani ako na deni kubwa inalipiwa pale, inakatiwa pale. Lakini hii mambo mengine kusema kwamba unajaza form-inakuwa mambo ya kujuana sasa. Kama hujulikani, basi unabaki ukiangamia na mtoto wako hasomi. Kwa hivyo unakuta wale ambao hawajiwezi wanzidi kugandamizwa. Kwa hivyo at least Katiba ya sasa izingatie maswala kama haya. Mengine mengi ninafikiri yapo katika hii memorandum.

**Com. Ratanya:** Asante sana. Okay, upeane hiyo memorandum yako Bwana Thomas. Na sasa tutaenda kwa yule anaitwa Fredrick Leshamta.

**Fredrick Leshamta Musuya:** Kwa majina ninaitwa Fredrick Leshamta Musuya, ni mkaji wa hapa. Pendekezo langu katika muundo ya Katiba, ni kwamba yafuatayo ningependelea yatiliwe maanani.

Kuhusu Executive, ningeonelea kwamba Rais apewe muda wa terms mbili. Terms zeneyewe ziwe ni miaka mitano mitano; kuwe na Waziri Mukuu ambaye atakua mwendeshaji wa serikali, Buge lipewe mamlaka ya kuchagua maCommissioners na Board of Directors, ama Directors na Executives katika parastatals. Ningeonelea kwamba Rais, kwa sababu ya kazi nyingi, asiwe Mbunge. Mbunge wa sehemu ile ambako anatuka-jimbo lile hupata taabu sana kwa sababu Rais utamukuta kwamba yeye huja kuvunja Bunge, ama anapofungua Bunge na wakazi wa pale watakuta kwamba hakuna anayewakilisha ama kuwapendekezea mapendekezo yao.

Pili, iwe wakati wa uchaguzi, uchaguzi wa Rais usiwe siku moja na ya Wabunge na local Councillors-kuwe na utaratibu kwa uchaguzi wa Rais. Siku yake iwe kando na kuwe na taratibu ya Wabunge na councillors wawe pamoja. Ya pili ni kuhusu ardhi. Ardhi katika Kenya imetuletea shida sana. Iwe kwamba kila mwananchi akubaliwe kupata ardhi pahali pale anapotoka. Kwa sababu utakuta kwamba jamii kubwa ya Kenya sa hii hata wale wanaishi mwambao wa pwani, utakuta kwamba kuna Mkataba ulioundwa na serikali ya ucolony-kabla hatujapata uhuru, ambayo sehemu kubwa inaitwa sasa ni ya Mazrui. Lakini ulikuwa mkataba wa mfalme ama Sultan wa Zanzibar na serikali ya Kenya. Wakazi wa sehemu hiyo mwambao ya pwani, ile ten mile strip, utakuta sasa wao wengi walijikuta masquatter.

Na kweli swali la squatter katika nchi yako mwenyewe ni taabu kubwa. Iangaliwe Katiba inapoundwa itie maanani. Sehemu zingine ni kuhusu hizi national parks ama reserves. Ikiwezekana, Parks ziangaliwe-Katiba iangalie ile sehemu kubwa ya wanyama ipunguzwe ili wale watu wa eneo hili ambao wanaitwa squatters, wagawanyiwe sehemu moja wapo-ili wapelekwe kwa makazi. Wanapopelekewa, wazingatiwe kwamba kitu ya kwanza ni maji. Wapelekewe mabarabara, mashule na hospitali.

Ya tatu ni kuhusu mazingira yetu. Mazingira yetu utakuta kwamba yameharibiwa-hasa sehemu zinazoitwa water catchment areas. Katiba itie maanani kwamba hizi water catchment areas, zilindwe na zi-ifadhiwe pamoja na wale wenyeji wa pale, ama elders wa sehemu ile ambao wanajua sehemu zile za water catchment areas. Wapewe uwezo zaidi kuzimiliki. Kwa sababu

utakuta watu wanakata miti ovyo ovyo na ndio maana unakuta sehemu nyingi tunapata shida ya mvua.

Rasilimali za nchi, yaani pato la nchi ambalo linapatikana kutoka kwa ardhi ama wapi, zigawanywe kitaratibu. Inapugawabyua ihakikishwe kwamba wenyeji wa pale kama kwa mfano mafuta imepatikana hapa ardhi ya hapa, wenye mji wa hapa, waambiwe kwamba ondokeni serikali imepata mafuta. Kwa kweli, kama ni mashini ama mafuta ikipatikana sehemu ile, mwenye ardhi ile pia awe na percentage ya share pale pahali-ama wenyeji wa pale pahali. Kabla serikali kuu kuchukua majukum uhakikishe kwamba-kama serikali itakuwa imeundwa iwe na majimbo, serikali ya majimbo ijulishwe kuhusu sehumu ile na serikali kuu ijulishwe ili ikuwe na percentage fulani hakayobaki pale.

Tatu, pengine ni kuhusu pensioners. Utakuta mtu anapo-retire serikali inamunyanyasa vilivyo. Taratibu za watu ambao wana-retire, serikali iaanze kufikiria kwamba anapo fika umri ule, basi iaanze kutengeneza marupuru yake yote hata siku ile ya kuondoka iwe anaondoka akiwa na marupurupu yake mkononi. Zaidi ya hapo ni kwamba kuna elimu, kiwango cha elimu; kiwe kwamba ni compulsory mtoto anapofika ule muda ya kuenda nursery, miaka minne ama mitano aingizwe nursery na mpaka Standard 8 iwe ni bure. Kama ni kulipa fee ianzie secondary-lakini iwe katika mapato ambayo watu wanaweza kujimudu. Kiwango hichi kwa sasa hivi kiko juu zaidi.

Ingine ni kuhusu ugawanyaji wa madaktari. Utakuta kwamba kweli kuna sehemu nyingi ambazo kuna madaktari kuliko sehemu zingine; na vifo ama nini vinatokea zaidi kwa sababu ukienda hakuna madawa hospitalini na madaktari ama wafanyikazi wakutosha-wale ambao wamehilimu, hawako. Zaidi ya hayo, ni kwamba ikiwa watu wataambiwa kwamba “wewe ni muja-kuja” na ume kuja pale, hii Chiefs Act, ipunguzwe nguvu. Kwa sababu utakuta kwa Katiba iliyopita, Chief akija akikuta State land ama akute trust land, wakiwa na watu tisa ama kumi anaweza kugawanyia mtu sehemu ile akae. Utakuta kwamba kuna sehemu kubwa zimefanya kulidhiwa na serikali. Utakuta lease ni ya 99 years na kweli sehemu ile haidumiwa na wananchi wanateseka. Napendekeza kwamba sehemu ile, Katiba iunde kwamba sehemu ile kwamba wapewe nguvu ya kuchukua ama kunyakua sehemu ambazo haziudumiwi, iili lease iwe cancelled, watu wagawanyiwe. Nafikiri yangu ni hayo.

**Com. Ratanya:** Asante sana Bwana Fredrick Leshamta, sasa ni Fredrick mwingine, anaitwa Pondo. Fredrick Pondo

**Fredrick Pondo:** Asante sana kamati, mimi kwa jina ni Fredrick Pondo mkazi wa(inaudible) Maoni yangu kama mwana Kenya, ni kwamba hapa Taveta asilimia kubwa-karibu wote ni wakulima. Na kama wakulima tatizo ambayo nigependekeza kwa Tume kwa Katiba ni kwamba wanyama wa pori wanatuingilia sana sisi wananchi wa Taveta-hasa zaidi katika location hii ya Chale. Na nikwamba wanyama walioko wengi hapa ambao wanatudhuru sana ni Elephants ama Ndovu.

Na mimi kama mwananchi wa Kenya ningependelea hawa Ndovu, kuna sehemu zingine za dunia ambao hawajui hata hawajaona Ndovu. Ingewezekana, kwa kuwa population ya hapa ni nyingi ya hizo ndovu, wangeuzwa na serikali ikiwezekana-wauze hawa ndovu ili idadi yao ipungue; na sehemu ambayo wanatokea ikiwezekana, izingiwe wire kabisa wasije

wakatuingilie. Hiyo ni point moja-hawa Ndovu.

Ya pili ni upande wa political parties. Mimi kama mwana Kenya ningependelea, mambo ya vyama vingi vinaleta ukabila. Ningefurahia kama tungekua na vyama viwili tu-ama ikizidi viwe vitatu-basi.

Ya tatu ni upande wa utawala. Mimi maoni yangu naonelea kwamba hasa huyu mtawala tuko naye karibu na ambaye ni Chief, awe akichaguliwa na raia na sio kuteuliwa. Kwa upande wa Wabunge, ningependelea mtu akingia Bungeni asifikiri kwamba ni nymba yake; awe at least kwa miaka mitano mitano mara mbili-kama Rais vile imependekzwa na wengi. Kwa hivyo Mbunge akiingia Bungeni, ajue atatawala kama miaka mitano. Akifauru kupita tena hiyo miaka mitano mingine, iwe ni ya mwisho asitarajie tena ya miaka kumi na tano ingine.

Upande ya watoto ningependelea kwa kuwa wananchi wa Kenya wengi tunajua kwamba watoto ni jamii ya watu wote. Lakini tunapendelea sana watoto wakiume na watoto wa kike hatuwapendelei. Ningependelea wakati wa ugawanyi wa ardhi ama mali, watoto wote wapewe usawa. Ya mwisho ni upande wa masomo. Tunaona kwamba watoto ambao sisi waKenya hasa walioko Taveta hapa, tunashindwa na kulipia watoto school fees kwa sababu ya kiwango cha school fees. Kwa saa hii ni hali ya juu sana. Kwa hivyo wale walioko secondary-ama ningependelea wale watoto, tume ijaribu kubadilisha ama irekebishe school fees kuwa secondary schools ziwe nafu ili mwananchi yoyote anaweza kua na uwezo wa kupeleka mtoto shuleni. Watoto wengi werevu wanashindwa kuenda shule kwa sababu wazazi wao hawana uwezo kwa sababu ya hali ya maisha. Asanteni sana.

**Com. Ratanya:** Na ya Primary?

**Fredrick Pondo:** Ya primary ningependelea iwe bure ingawaje si bure, lakini at least iwe bure.

**Com. Ratanya:** Asante sana Bwana Fredrick. Twende kwa Kassim Leshamta.

**Kassim Leshamta:** Kwa jina naitwa Kassim Leshamta nashukuru kwa ajili ya Urekebishaji wa Katiba mwaka huu. Kama mimi ninavyoelewa, Kenya ina makabila zaidi ya arubaini-na kuna makabila makubwa na madogo. Nilikuwa naomba hii serikali na hii Katiba ijali masilahi ya kabila ndogo kwa sababu kuna kabila ndogo. Kama sisi Wataveta hapa, sisi ni kabila ndogo. Wakati wa kuchagua Mbunge awe ni Mtaveta. Taveta inaeleweka kwa(inaudible)na ukulima; Watu wengine wanakuja kufanya kazi, wanafanya biashara-ni hapa; wakati wa kuchagua Mbunge hawatachagua Mtaveta wakisema kwamba ukichagua Mtaveta atatufukuza hapa sisi masquatter. Kwa hivyo nilikuwa naomba katika urekebishaji wa Katiba hii, mwenye kupigania Ubunge au uCouncillor awe ni mwenyeji, Mtaveta mwenyewe-sio mtu wa kutoka nje. Hiyo ni moja.

Ya pili ni mambo ya ardhi. Utakuta mtu ametoka mbali hajulikani ametoka wapi; Hii mambo ya Chiefs Act. Anuruhusiwa

MKenya apewe makao. Sasa Chief atumie ile sheria ya kwamba, huyu mtu ametoka huko-mzee mzima kama mimi nina watoto kumi, na ngombe na matingatinga ya kulima; Huko nilikozaliwa, mpaka miaka leo sitini nilikuwa ninakaa wapi? Na kile kilicho nitoa huko ni kitu ni gani-hawezi kuuliza kitu kama barua ya Chief kutoka kule kwake; Na ukija kubebana na mtu kama huyo tena anakunyanyasa-ana mali na wewe huna mali. Kwa hivyo pia, hiyo Chief's Act ipunguzwe na hawa wageni wachunguzwe kwa sababu wako wengine wamekuja hapa wanatusumbua mpaka wengine wanuwa watu nyumbani kwetu. Kwa hivyo hayo makao wapewe kihalali kwa sababu ni WaKenya-zile sehemu za serikali, sio sehemu za wenyeji.

Na. Juu ya Ndovu, watu wngine tunakaa njaa hapa kwa sababu ya hao ndovu. Tunalima, tunapanda mahindi ikishako maa, ndovu wanakuja; ukiua-utaenda dunia gani ya Mungu? Sereikali itupatie ruhusa na sisi tuwae (grumbling from the audience)------eeh sasa mimi nitakfa kwa njaa na huyo ndovu-----na serikali haitupati chakula. Hatuo ndovu wapunguzwe ama tupewe ruhusa na sisi tuwaue. Yangu ni hayo.

**Com. Ratanya:** Asante kwa hayo maoni yako, na tutaendelea kwa huyu Lavu Muthunu.

**Lavu Muthunu:** Mimi kwa jina naitwa Lavu Muthunu. Yangu ni kusisitiza habari ya hawa Ndovu. Wamesumbua watu miaka mingi; mara unaambiwa ikiharibu mimea yetu utalipwa- hakuna kitu tumelipwa. Yangu ni hayo. (Laughter from the audience)

**Com. Ratanya:** Asante Bwana Lavu kwa hayo maoni. Unataka ulipwe compensation? Okay hiyo tumesikia. Tuende kwa Christine N. Keah.

**Christine N. Keah:** Kwa jina naitwa Christine Keah. Maoni juu ya Katiba. Kwanza msaada inapotolewa ipitie kwa Council yetu na iwe ina kamati ya wenyenji wa hapa-msaada wowote kutoka nje ama kutoka kwa serikali.

Pili, Katiba iangalie wakina mama wapate viti vingi Bungeni. Kwa upande wa nominated, wajazie-jazie wakina mama hapo na kazi pia wasibaguliwe. Tatu, kulingana na wizi wa sasa, Katiba ipitishe mtu atakaye ua anyongwe-bila kufungwa. Nne, watoto wafanyie interview hapa hapa Taveta na iwe ni wenyeji wa hapa bila kubagiliwa kwa sababu, watoto wanatoka hapa, wanaenda wilaya ya Wundanyi, wame pita wako na ma B's wako na C+, watoto wanfika pale, unakuta watoto wanaenda kama ni sitini na hakuna mtoto hata mmoja anapekelewa. Kwa hivyo interviews zirudi nyumbani.

**Com. Ratanya:** Za kazi ama gani?

**Christine N. Keah:** Interviews za kazi. Tano, wakina mama wanapata taabu sana wakati wakizaa-hospitali iko mbali, vifaa vya kutosha pia hakuna na madaktari ni wachache sana. Sita-ya mwisho, Mbunge anayechaguliwa kama hapa Taveta tukiwa na makabila mengi, tunaomba awe ni mwenyeji wa hapa hapa na awe Mtaveta"full stop" (Laughter from the audience)

**Com. Ratanya:** Okay Christine hiyo kweli ni full stop, na uandikishwe hapo. Sasa, tumesikia hiyo full stop ya Christine na tuendelea sasa tuone mwingine anaitwa Flora Sumaku.

**Flora Sumaku:** Kwa majina yangu mimi ni Flora Mwanamiti Sumaku. Maoni yangu ningemunga Christine mkono kwa ajili ya Mbunge.

Kusema cha kweli tunaomba Mbunge wakati tuna wakilishi Bungeni wakati linapo kaa waangalie Mbunge achaguliwe kwa sehemu hiyo hiyo yao-kwa mfano hii yetu ya Taveta.

Ya pili, ninaomba wakina mama wakati wanapofiwa na waume wao wasirithiwe, kwa sababu magonjwa ya ukimwi yame kuwa ni mengi. Tatu, ninaomba kwa upande wa shule, kama shule za high school, shule za primary-garama ya shule ipunguzwe kwa sababu watoto wengi wako manyumbani, wamekosa school fees na ni hapo hapo utakuta watoto wanakua chokora. Maoni yangu ni hayo tu.

**Com. Ratanya:** Asante kwa hayo machache Flora na mwingine anayofuata ni Rita Namche Rama.

**Rita Namche Rama:** Kwa majina mimi ni Rita Namche Rama. Mimi ningesisitiza sana habari ya ubakaji wa watoto wa kike. Kwa kweli sisi wazazi huwa tunaona uchungu sana. Mtu akibaka mtoto yoyote wa kike, afungwe maisha.

Na lingine ni kama mtu akiharibu mtoto wa kike akiwa shuleni, huyo mtu alazimishwe kuchukua huyo mtoto na fine alipe-garama yote ya school fees atoe. La si hivyo, akikataa kumuoa, afungwe na garama alipe; maanake sisi wazazi tunasomesha watoto kwa shida sana.

Na jambo lingine la pili, ni mtu kama akiamua kuoa mke wake wa pili, ile mali ametafuta na yule mke wa kwanza, apatiwe yule mke wa kwanza-yule mwengine atamutafutia mali yake kando. Yangu ni hayo.

**Com. Ratanya:** Okay Rita hayo yanatosha twende kwa Crispus Ayelo Musuya, Crispus uko?

**Crispus Keah Leshamta:** Kwa majina mimi naitwa Crispus Keah Leshampta Musuya. Kwa maoni yangu kuhusu Katiba tutakayounda, tuwe na Rais ambaye ana mamlaka, ambaye amechaguliwa na wananchi wote kwa asilimia hamsini na moja. Na kwamba huyo Rais awe na uwezo wa kuunda serikali ambayo itakuwa na Waziri Mkuu kutoka kwa chama kitakacho shinda Wabunge wengi.

Uchaguzi wa Rais uwe siku tafauti na uchaguzi wa Waunge na wale wa macouncillors ili kama itakua ni kurudia uchaguzi kwa kupata asilimia hamsini na moja, pasiwe na kurudia kwa UBunge tena, ni hawa watu wawili watokao gombania-yule wa

kwanza na wa pili. Katika utengelezaji wa kazi za serikali Rais awe ndiye Executive Officer-mkubwa na katika baraza la mawaziri, yeye ndiye atetua baraza lake hadi Attorney General. Kuwe na serikali ya majimbo, kuwe Chairman wa jimbo atakaye chaguliwa na wananchi na yule mutekelezaji wa jimbo awe anateuhwa na Rais.

Tukija katika wilaya vile vile pasiwe na serikali mbili. Kuwe na serikali moja ambayoni ya wilaya ambaye Chairman wake anachaguliwa na wananchi, mtekelezaji wake mkuu awe anateuliwa na serikali kuu na macouncillors wa sehemu hiyo. Pasiwe na DC ambaye ana council tafauti. Iwe ni Council hiyo hiyo, ndio hiyo inakuwa na mtekelezaji mkuu. Katika tarafa kuwe ni hivyo hivyo-pawe na macouncillor wanatoka katika location na hawa macouncillors ndiyo watakuwa Chairmen wa maendelo ya ile location na wale machief wa sasa ni watekelezaji wakuu.

Kwa hivyo kutakuwa na baraza moja na location ambaye Chairman wao ni councillor wao. Katika vijiji, vigawanywe kwa sababu ya security, pawe na wazee wa nyumba kumi kumi ambao wanapewa mamlaka kamili kulinda sehemu yao. Utungaji sheria uwe mkononi mwa wale ambao wamechaguliwa na wananchi-lakini katika wakati wa emergency, Rais awe na mamlaka ya kutanga sheria zake. Na vile vile katika kudhumisha sheria zingine kama upande wa police, pasiwe na maCommissioner wawili kama iliyo sasa hivi. Kuwe na Commissioner mmoja wa police ambaye-jeshi ambalo linaitwa AP sasa liunganishue na Commissioner mmoja-huyo wa Kenya Police. Ma-baraza na majimbo yanayo haki ya kuwa na uteuzi wao.

Kuhusu haki; Kuna mikataba mingi ya kimataifa juu ya kulinda haki za watu binafsi. Lakini kwa sababu fulani na fulani, hizo sheria zinavunjwa hasa hata kwa upande wa wandishi. Pawe na uwezo wa Rais kutunga sheria za kuzuia uhalifu wa wandishi. Kwa sababu hawa wandishi upotosha serikali nyingi. Habari ni haki ya kila mtu; kupata habari ni haki ya kila mtu lakini hiyo habari iwe na vikwao vyake isije ika(inaudible). Upande wa uraia: Hapa Taveta tunapakana na makabila ya nchi zingine na tunawafahamu. Wale wake watu tutakaowaoa wawe wakithibitisha kawamba wameolewa kihalali, wapewe kibali cha uraia bila kupitia vikwazo vingi.

Tukija upande wa ardhi, sehemu au ardhi yote iwe chini ya mamlaka ya wenyeji pale. Tunasikia kuna mambo ya State land, kuna Trust land, kuna Private land. Sasa Trust land ilikuwa ni ya wananchi lakini ilitwaliwa vibaya na watawala. Kwa hivyo tunataka wananchi waruhusiwe kumiliki ardhi yao na ile ambayo ilipeanwa kimakosa, waruhusiwe kui-claim- kudai ardhi yao iliyo chukuliwa kimakosa. Mashamba makubwa makubwa ambayo hayatumiki ipasavyo-Private land, Rais awe na jukumu la kuchukua sehemu na kugawanyia wenyeji wa pale. Ikiwa ardhi-mtu amechukua ardhi kwa nguvu bila idhini ya wenyeji pale, awe anaweza kushtakiwa na swala la squatter liondolewe kabisa. Hakuna sababu ya mtu kuwa squatter-akivamia ardhi ya mtu ashtakiwe mara moja. Sio mtu awe amehama kwake aje kukaa kwa ardhi ya mtu mwingine aseme ni squatter-apelekwe mahakamani. Kuwe na sheria mahususi ya kuzuia watu kuhamia ardhi ya watu.

Upande wa mila na desturi, makabila madogo madogo yamenyanyaswa na makabila makubwa kuvamia sehemu zao na kuukalia na kuchukua viti ya Ubunge, viti vya ucouncillor- sisi hapa tuko mpakani; watu wanafukuzwa katika nchi ingine kule

kwa uhalifu wao, wanakuja hapa wakiwa ni Wakenya walindwe-wanapatiwa ardhi ya Taveta. Watu wanashindwa kwao kuania Ubunge huko kwao, wanaleta watu wa kwao, wale wameshindwa nao wanakuja hapa wanavamia sehemu ambayo ni Private land wanaruhusiwa kupiga kura. Jambo la kura inafaa kuhakikisha kwamba hakuna mtu anahamia sehemu ya mwenzake- kura isiwe ya kuhama-hama. Kura iwe ni permanent issue-sio watu kuhamia ama kubadilisha wanavyotaka-kwa sababu wengine wao wanashindwa kwao, wanahamisha watu wao na kuleta watu wao hapa. Tunaomba serikali ihakikishe kwamba makabila machache ama watu wandogo wandogo, wamelinewa ki-Katiba kuhusu mila zao na haki zao za kimilika ardhi yao.

Upande wa elimu, ni kwamba elimu ya sasa haifunzi wanafunzi uwezo wa kujitawala wenyewe badaye. Ninapendekeza kwamba elimu, watoto wafundishwe vafaa ambazo zinawaweza (inaudible) badayeawe na uwezo wa kutengeneza mwenyewe kama vile ilivykuwa zamani-unafunzwa kujenga, unafunzwa kuchora.

**Com. Ratanya:** Asante Crispus, umechukua muda lakini maoni mazuri. Tuende kwa Nguruwi Karitei.

**Nguruwi Karitei:** Hamujambo? Mimi katika maoni yangu si mengi sana ni madogo. Kusema haki, hapa Taveta kitu kinacho tuhusu kabisa kabisa hapa tunavyonea kabisa kabisa ni ndovu. Ndovu wametutia njaa katika mwoka wa elfu mbili na moja-kwa njaa iliyo kuwa mwaka wa elfu mbili na moja. Kingine ni kwa mipango ya wananchi. Hapa kwetu tunaambiwa kila saa, kila mwaka, tutachagua Wabunge, tutaletewa lami kwa barabara-lami, lami, lami mpaka wa leo-hatujaiona.

Lengine, hapa Taveta majambazi wamezidi; kuua watu na kunyanganya watu vitu zao ndani ya nyumba. Hio ingekuwa kwamba serikali ingekuwa na msaada, watuletee watu wa kuchungua mambo kama hayo. Mimi kwa hayo sina mengi ni hayo tu, iliondani ya kichwa yangu.

**Com. Ratanya:** Sasa nitaenda kwa Pascal K. Hussein. Tumepita mmoja, hebu tuende kwa Margaret kwanza. Nilikuwa nimepitia Margaret N. Ngurini.

**Margaret N. Ngurini:** Asante. Mimi nasalimia kiTaveta. Mnisamehe, nasalimia kiTaveta, mu-meamuk aje?

**Translation:** Huyu mama anasema hivi; kwamba kwanza mambo ya Ubunge: Anasema Taveta watu wanakuja wanapewa Ubunge, hata wenyeji hawa wajui wanatoka wapi. Mambo kama hayo yanawatatiza wenyeji wa hapa-Ubunge upewe mtu wa hapa hapa-mwenyeji wa hapa hapa.

Ya pili anasema mashamba; Mashamba makubwa yalichukuliwa na wazungu na sasa wameondoka bado wenyeji hawarudishiwi, wanambiwa wanunuwe. Kwa nini na ni ardhi yao? Anasema maneno yake ni hayo hayo amesema na zaidi, anasisitiza tu jambo la mtu mgeni kuja kugombea uongozi wa sehemu hii-haoni kama ni sawa.

**Com. Ratanya:** Okay mwambie mama ni asante sana, tumesikia hayo. Sasa tutaenda kwa Pascal K. Hussein.

**Pascal K. Hussein:** Majina yangu ni Pascal Hussein na nina maoni kadha wa kadha. Kwanza ningelipenda hasa kuzungumzia kuhusu uchaguzi. Ningelipendelea kwa maoni yangu kwamba, uchaguzi wa Wabunge hasa watakao chaguliwa, waweze kuwa wanapitishwa na asilimia zaidi ya hamsini ya wakaaji wote wa eneo lile. Na ni kwamba pia katika Katiba, kuwe na sheria ya kwamba kama yule Mbunge aliyechaguliwa, ama Councillor atakayechaguliwa, kama hataweza kuhudumia wale wananchi ipasavyo-kwa ile mifano ambayo tunaona hivi sasa ambayo inaendelea katika Bunge letu, kuwe na sheria ya kwamba waweze kuondolewa kazi ile kwa kupitia public opinion polls ili ile sehemu iweze kupata Mbunge mwingine ambaye ataweza kushugulikia masilahi yao.

Katika community based services kwa mfano, tuna National Youth Service, tuna Armed Forces-katika nchi zingine ninaweza kutoa mfano wa Ethiopia, National Youth Service hutumika kutengeneza mabarabara ya nchi zile, Armed Forces pia hutumika kutengeneza mabarabara ama hospitali kwa hivyo hapa kwetu nigelionelea pia watu kama National Youth Service, Armed Forces, watumike katika construction ya mabarabara, bridges hata hospitali kuliko serikali kutoa contract kama zile kwa watu ama macompany mbali mbali na kutumia pesa ama rasilmali za nchi kwa kuchukuliwa kuenda nje.

Kuna jambo lingine ambalo pia tunaweza kusema kama ya Foreign affairs policies. Serikali ama Executive hutoa maoni yao ama u-sign policies fulani fulani kwa niamba ya nchi. Kwa mafano, tuna-sign mambo ya Comesa, tuna-sign mambo ya PTA-Preferential Trade Areas, East Africa Cooperation bila kuangalia masilahi ya wale wananchi ambao ile mikataba tutakayo sign inawahusu. Naweza kutoa mfano ambao ulitendeka na ambao hivi sasa unauchumu ama unasumbua wananchi wadogo wadogo.

Kama huu mkataba wa East African Cooperation, ambao ingekua ni free trade. Kwa hivi sasa wakulima ambao wanahusika na kilimo cha mazao wanapata matatizo kwa sababu vitu vya kutoka nje vinakuja vina-flood market na vina-render those people financially bankrupt kwa sababu, mazao yao hayanunuliwi. Vitu vya nje vinauzwa kwa bei raisi-na umaskini unazidi. Kwa hivyo poverty eradication ni kama hakuna katika Kenya.

Kuna pia trade union representation-wafanyi kazi. Katiba ingefaa kusema ya kwamba, ama iwekwe kwamba representation ya wafanyi kazi, yaani trade union, ziwe ni za lazima. Ili iwe mfanyi kazi asiweze kunyanyaswa na matajiri na pia pale, wale wastaafu ambao watastaafiswa baada ya umri wao kufika, wawe enshirined katika ile Katiba kwamba watatewe mpaka hata wakati watakapo toka. Kwa mfano, utakuta mzee labda alifanya kazi kwa miaka arubaini na tano katika serikali na aka-retire. Anapatiwa pension ambayo hivi sasa hata kilo ya sukari hawezi kununua nayo. Kwa hivyo iweze kuangaliwa kwamba, vile miaka inavyoendela na hao pia wanaweza-masilai yao yanaweza kuangaliwa; Because they wasted a lot of their years working for the Government or for the country as a whole.

Yangu lingine-nafikiri ni la mwisho, ni kuhusu discrimination of small communities. Kwa mfano, tuna makabila arubaini na tatu katika Kenya na hayo makabila yana right ya kuwa katika Kenya. El Molo ni kabila ambalo labda kwa kipindi cha miaka tisini walikua mia mbili na arubaini. Wale watu pia wana haki ya kuweza kuwakilishwa katika Bunge. Kwa hivyo Katiba iweze kuundwa ya kwamba makabila yote katika Kenya, yaweze kuwa equally represented at a national level-decision making ya nchi ili cultural issues zao ziweze kuwa represented equally. Na tuseme kwamba pia hizo small communities, ziwe ziko represented politically and administratively. Administratively mimi na sema from grassroots; kwamba kuanzia mzee wa mtaa kuja kwa ma-chief Manaibu wa Chifu, ma-Bunge-wote waweze kuingizwa katika hii-that is to safeguard those small communities. Nafikiri yangu muhimu katika leo ni hayo. Asanteni sana.

**Com. Ratanya:** Okay, sasa tuende kwa anayefuata, ambaye tunamwita Hutesima M. Hamed.

**Hutesima M. Hamed:** Kwa jina mimi naitwa Hutesima Muhamud Hamed. Maoni yangu ya leo, ya kwanza ni elimu ya msingi. Elimu ya msingi iwe bure. Mtoto hasiitishwe kitabu, mzazi asiambiwe ajenge jengo lolote, mtoto hasiitshwe text book, mzazi aitishwe school uniform peke yake na pencil kama zamani.

Ya pili ni matibabu yawe bure. Mtu akienda hospitalini atibwe bure na tena kuwe na dawa hata damu. Ya tatu ni mashamba. Shida kubwa kubwa sana iliyoko hapa Taveta watu walipata ni kuwa up-country mashamba yakipimwa, watu wakipatiwa title deeds Taveta walikatazwa kupatiwa ndio unaona mashamba mengi Taveta yamevamiwa. Katika hiyo hiyo mashamba, wale wamezaliwa na wamefikisha miaka kumi na minane na hawana mashamba wa pewe mashamba katika national parks ambazo ni kubwa kila mtu acre kumi bure.

Lingine ni pension: Mzee aki staafu ama kabla kustaafu,pengine amefariki amemuacha mama na watoto na watoto wanasoma, anasumbuliwa hapatiwa pesa za NSSF, hapatiwi pesa za pension, mama hajui yale maofisi na pengine ameolewa kimila-anazidi kusumbuliwa. Ingine ni Rais; Katika maoni yangu mimi, naona Rais hafai kuwa above the law. Inatakikana Rais akifanya kosa lolote ashtakiwe na mahakama iwe na uwezo, Bunge liwe na uwezo wa kivyake na serikali iwe na uwezo wa kivyake. Hivyo ndivyo vitakvyokuwa pamoja.

Nominated MPS; Katika maoni yangu mimi naona hawa nominated MPS tayari ni watu wame toka kura wameanguka, halafu serikali-mtu anarudi anawachagua pamoja na ma-councillor, sisi, raia ni watu tumewakataa, wanarudi wanachaguliwa tena, wanakuwa nominated-wanapatiwa tena mishahara mikubwa ambayo ingelipa watu wengine na lote wanapewa U-Minister.

Siku ya uchaguzi; Siku ya uchaguzi katika maoni yangu ningependela vyama.kama cha Kanu, DP, SDP, uchaguzi wote ufanywe kwa siku moja. Kwa kuwa ni wale watu wanakwenda wanachagua mtu kwa DP wanarudi tena-wale wale watu wanarudi wanachagua mtu kwa kwenu ni wale wale watu kwa sababu siku ziko tafauti. Unakuta mtu mmoja anachagua karibu

watu watano hata yeye hajulikani ako katika chama gani.

Ya mwisho ni wafanyi kazi wa serikali na masharika. Wafanyi kazi kweli wamenyanyaswa sana unakuta umeandikwa kwa muda mrefu, hakuna promotion, hakuna ku-move job group, hata wewe mwenyewe unakatwa pesa zako za National Insurance Fund hakuna usaidizi wowote unapata manake zile hospitali unaruhusiwa kwenda hazina dawa. Nimemaliza. Asanteni.

**(Question from one of the Commissioners):** Una taka tufanye aje?

**Hutesima Hamed:** Our civil servants? Our civil servants wanatakiwa waongezwe mshahara, sio walimu peke yao na kulingana na vile mipangalio iwe pia wanakuwa promoted si ati mtu anafanya kazi miaka ishirini bado ako job group F. Hawana promotion, hakuna mishahara haiongezwi, house allowance haiongezwi.

**Com. Ratanya:** Okay, asante sana Mohamed kwa hayo maoni mazuri. Sasa tutaenda kwa, anayofuata ni Fasigol Lelegeshu. Okay.

**Fasigol Lelegeshu:** Mimi kwa majina ni Fasigol Lelegeshu. Maoni yangu kuhusu kazi ya kurekebisha Katiba leo tarehe tatu, mwezi wa tano, mwaka elfu mbili na mbili, ni kama ifuatavio.

Kwanza kuhusiana na Katiba, Bunge ziwe na uwezo wa kubadilisha sehemu yoyote ya Katiba bila kuhusisha wananchi kama inavofanyika sasa. Kuhusu uraia, serikali isiruhusu uraia wa mtu katika nchi mbili tafauti. Kuhusu usalama wa taifa, uandikaji wa kazi za jeshi na askari uzingatie usawa katika kila kabila la Kenya. Kuhusu utaratibu wa uchaguzi, serikali ihakikishe kwamba makabila madogo yote ya Kenya yamepata uwakilishi Bungeni. Kuhusu haki ya ardhi, jamii na watu binafsi wenyeji wa eneo hilo wawe na haki ya kumililia wa ardhi yote mahali hapo, kando na ile inayo milikawa na serikali. Kuhusu ujira sereikalini, serikali ihakikshe kwamba kila kabila la Kenya linangaliwa katika ajira za kazi mbali mbali za serikali hasa za utawala. Haki za utamaduni; Tamaduni za wenyeji asili la eneo hili iheshimiwe. Haki za kimusinigi; Serikali ihakikishe kwamba kila mtu amepata elimu ya msingi kwa lazima na iwe ya bure. Mali ya asili; mali asili iliyo katika eneo fulani, iwafaidi wenyeji wa eneo hilo moja kwa moja kwa kiwango fulani nimekomea hapo, asante.

**Com. Ratanya:** Okay, sasa tuendelee kwa anayefuata, ni Alexander Lelegesu. Alexander uko karibu? Ulikuwa hapa tena? Okay endelea.

**Alexander Lelegesu:** Mimi kwa majina yangu naitwa Alexander Lelegesu ni Mtaveta, na yafuatayo ndio maoni yangu kuhusiana na urekebishaji wa Katiba. Maoni yangu ni kwamba pensioners-wale wafanyikazi ambao walikuwa wanafanya kwa serikali, walipwe marupurupu yao mara moja baada ya kuwacha ihazi.

Maoni yangu mengine ni kuhusu utabibu. Utabibu uwe wa bure si kama sasa ambapo watu wengi wanafariki nyumbani kwa sababu ya ukesefu wa pesa za kwenda kwa utibabu. Linalofuata ni kwamba ma-Chiefs, Assistant Chiefs, Councillors wachaguliwe na wazalendo wa sehemu abayo anatoka na pia awe ni mzalendo. Ubakaji; Anaye baka .msichana-rape, afungwe miaka kumi. Urithi; Urithi uwe sawa kwa watoto wote wa kiume na wa kike. (inaudible)majadiliano ya Bunge yawe moja kwa moja; si kama sasa ambapo inapitia kwa viombo vingine, halafu unaambiwa Mbunge wako amasema hivi na vile.

Ya kufuata ni kwamba pahali pa kuabudu kiasili kama kule Lake Challa ambapo kwa jina lingine panaitwa Nakuruto, Kidong, Mukuni pasichukuliwe au kuuzwa kwa mtu au kwa kundi la watu maana pahali pale ni pahali patakatifu kwa jamii ya ki-Taveta. Pahesimiwe na Katiba na patengwe kwa jaami hiyo. Ya kufuata ni kwamba vagrant Act irudishwe kama beleni kwa sababu kuna wengi ambao wanatangatanga huku na huku na hakuna chombo cha kuweza kuthibitisha.

La kufuata, kila kabila iwakilishwe Bungeni. Sio kama hivi sasa ambapo makabila mengine inatoka huo ina kuja kunyakua viti za uBunge katika sehemu ambazo hawatoki. Ya mwisho ni kwamba mtu anayetaka UBunge sharti apitiae katika ile Njama katika Taveta. Hayo ndio ninayo kwa sasa. Asante.

**Com. Ratanya:** Okay. Asante Alexander na hapo tunaenda kwa Sophia K. Ngoi.

**Sophia K. Ngoi:** Kwa majina naitwa Sophia Kimboi Ngoi. Yangu ninayo sema kwa upande wa Katiba, nasema serikali ipige marufuku soko uhuru kwa sababu inatuharibia biashara.

Ya pili; Kuhusu shule za secondary, fee imekuwa kubwa mno, Katiba ipunguze hii. Tatu; Mbunge au Councillor awe mwenyeji wa hapa-yaani Mtaveta. Nne; College pia fee iko juu sana. Unasomesha mtoto pia akimaliza college hapati kazi, huo ukabila tunaomba uishe kwa sababu ubaguzi uko mwingi sana. Tano; Mzazi anaye mpiga mtoto hadi afe, afungwe maisha. Yangu ni hayo.

**Com. Ratanya:** Asante sana kwa hayo machache Sophia na hapo tuende kwa Agnes K. Makuna.

**Agnes K. Makuna:** Mimi kwa jina naitwa Agnes Makuna. Mimi kitu ninacho omba, naomba kwa wazazi wote wa kiume mpaka wa kike, tunapo patiwa mtoto wa mtu, mtoto ameoa ameleta msichana wa watu kwangu mimi namufanya kama maid. Hiyo pia tunaona inadhuru watoto sana. Na pia yule msichana ameolewa katika huo mji akapokelwa kwa furaha, anazidi kunyanyasa ule mji na pia kunyanyasa yule mama mzee. Akiwa bwana wake yuko hapo nyumbani, ndio anadanganya ndanganya huyo mama mzee. Akiwa bwana wake ametoka, huyo mama huteseka anaweza kushinda njaa kutoka ashubui mpaka jua litue na matusi juu yake. Sasa naomba watoto warudie kile kizamani-kuheshimu wazazi na pia wazazi waheshimu wale watoto wa watu wameolewa hapo katika huo mji. Yangu ni hayo.

**Com. Ratanya:** Okay. Asante Agnes na kwa hivi sasa tutaenda kwa Leshamta Nguruwi.

**Fredrick Leshamta Ngruwi:** Kwa majina najulikana kama Fredrick Leshamta Nguruwi, mimi ni mkaaji wa hapa Challa. Upande wa Katiba, ambayo tunashukuru serikali ilivyo tupangilia iletwe kwa wananchi, mimi ninanza na ardhi.

Upande wangu naonelea ardhi inatakikana mwenyeji ambaye ni asilia wa pale awe na uwezo wa kumiliki hayo mashamba makubwa makubwa kwa asilimia arubaini. Mbuga na mali asili pia mwenyeji aruhusiwe moja kwa moja kuamua anochotaka kifanyike pale. Hilo litatoa matatizio kama hayo tunakuta Ndovu wanaingia na kuharibu mimea ya wananchi.

Upande wa Mbunge; Mbunge, ama tuseme mwanasiasa yote yule awe ni mwenyeji asilia wa pale-asiwe ni wa kutoka nje. Kizazi chake kiangaliwe kwamba kuanzia miake sitini na tatu, kiwe kilikuweko katika eneo lile. Jambo lingine ambalo liko ndani ya serikali na linatatiza watu, ni hii mambo ya cost-sharing. Hili ni jambo ambalo limeumiza wananchi ambalo limengia mpaka mahospitaini, shuleni na unakuta shule ikisemekana kwa mfano primary schools ni free, lakini still mzazi ama mwanchi anazidi kuumia. Kwa hivyo mzazi wa kiwango cha chini-maskini sio raisi na unawakuta machokora wamazidi kutokana na hali hiyo. Kwa hivyo hiyo cost-sharing iondolewe na elimu iwe ya bure, Primary, Secondary iangaliwe kile kiwango kipunguzwe pamoja na colleges. Na kwa(inaudible) Secondary Schools-cost sharing schools ziwe leo, Government Secondary Schools-isiwe pamoja kwa sababu unaweza kukuta private iko sawa sana na some of the Government schools. Sasa unakuta mwananchi anaamua tu kutoa mtoto pale anampeleka shule za private ambazo pia saa ingine kiwango kiko chini----

Ningependelea pia kuwe na serikali ya majimbo. Hii upande wangu naonelealea kwamba hii serikali ya majimbo, itajaribu kuleta usawa ndani ya mikoa ambayo itajaribu kumifikia ule mwananchi wa kiwango ya chini sana. NGO's na masharika haya.ya serikali, ningeonlea ya kwamba hayo mashirika sana sana tukichungaza hapa Kenya, yanalemea upande mmoja zaidi. Unakuta kama hapa Taveta mwaka huu--- Utawala; Upande wa utawala, mimi ningeonelea Rais achaguliwe na wananchi wote na asitoke katika chama chochote kile. Asitoke katika chama chote kile. Katika utawala huo, pawe na Waziri Mkuu ambaye yeye ndiye atakayetaka katika chama na awe amepita katika asilimia isio pungua hamsini na moja katika nchi nzima.

Upande wa Mbunge; pia na Councillors-ama wacha nisungumze kabla nirudi pale pale- lakini tukija kwa Chief, mimi ningeonelea kusema tuna muchagua Chief ni sawa na kuweka utwala katika siasa na ni vitu viwili tofauti. Kwa hivyo machief wawe wanateliliwa, lakini, wateuliwa kutoka sehemu ile ile. Hiyo ni pamoja na Sub-Chiefs. Wanaweza kuteuliwa kuungana na area DO na wazee wale ambao walikuwa wamechaguliwa katika kijiji.

Local leaders-hawa wazee wa mtaa-hao ndio tunaona wachaguliwe na wananchi wa sehemu hiyo na katika hiyo local leaders, pawe na wazee pia wa nyumba kumi kumi. Hii ni kwa sababu ya usalama wa nchi kwa sababu pame kuwa na wageni wengi na ni hatari; mtu anaweza kuingia hiyo sehemu na hajulikani. Sasa wale wazee wa nyumba kumi kumi ni rahisi kuelewa kwamba ni nani ameingia katika .kijiji chake na akajulikana. Uenezaji wa habari; mara nyingi tumejaribu kuyafikia mambo ya

kizungumzwa katika radio, magazeti- kinyume na vile yalivyo. Patokee sheria itakayalinda uenezaji wa habari ili, lile lakuangusha hali ya pahali, mwenye kuandika hiyo report achukuliwe hatua mara moja.

Unyakuzi wa Ardhi; sehemu nyingi katika Kenya watu wamekua wakililia unyakuzi wa ardhi, unakuta public areas inachukuliwa-tafadhali hapa tulikuwa tunaomba sheria itoke kali sana ili sehemu hizo-hata kama ni nani alinyakuwa hiyo sehemu, anyanganywe na afidie.

Makabila madogo madogo; Katika hali ya Kenya tungeliomba haya makabila madogo madogo, ya wakilishwe. Hii ni kumanisha kwamba ikiwa Wabunge wa teule-wanaoteuliwa- inawabidi wateuliwe, watoke katika haya makibila madogo madogo yasio kuwa na wakilishi ndani ya Bunge.

Wafanykazi wa serikali na mashirika; hawa wafanyakazi wa serikali na mashirika, imeonekana wanaendeleza sana ufisaidi kutokana na kupelekwa pahali na kukaa muda mrefu. Kwa hivyo ingekuwa miaka kumi peke yake inamtosha yule mtu kukaa pale, ikisha ahamishwe aende pengine. Hii itafanya ufisadi ndani ya ile sehemu ipungue.

La mwisho, ni kuhusu wanasiasa wa kuhama-hama. Pawe na sheria ya kuwalinda. Mwanasiasa akiingia kwenye chama asitoke pale baada ya uchaguzi mpaka mwaka uishe. Hii inaleta usupuvu ule unatokea ndani yake. Nashukuru.

**Com. Ratanya:** Okay, hapo ni asante sana Leshamta na tunaenda sasa kwa mwingine na ni Eleizabeth N. Mbele.

**Elizabeth N. Mbele:** Kwa jina mimi ni Elizabeth Mbele, hiyo "N" inamanisha Nashelengai Mbele-Elizabeth Nashelengai Mbele, Mtaveta, mkaaji wa Challe.

Sasa hapa nina memorandum ya kikundi, lakini, ningeongeza yale ambayo yako kwa memorandum-sijui kama naruhusiwa nisome memorandum yote, ama niongezea yale ambayo naongeza juu yake.

Katika hii memorandum kuna jambo la kuhusu elimu kwa huu urekebishaje wa Katiba, hili jambo la elimu ningependelea kuwa elimu ya msingi iwe ni ya bure. Elimu ya secondary kiwango chake kiwe cha chini ambacho mwananchi wa kawaida anaweza kulipa. Elimu ya chuo kikuu iwe kama zamani, yaani wanafunzi wapatiwe scholarship. Malipo ya college yapunguzwe kwa sababu, sio hakikisho kuwa ukipeleka mwanafunzi katika college atapata kazi. Wizara ya elimu igaramikie garama za mwanafunzi kama vile zamani; eg. Vitabu, kalamu, chalk na mengineyo.

Ajira; yaani kazi; Kazi itolewe kwa usawa bila ubaguzi kwa kijinsia, kikabila au kielimu. Kupandishwa cheo kazini au kwa mashirika kuwe bila ubaguzi wa kijinsia au kikabila au kielimu. Kwenye mahojiano ya kuchagua wakufunzi wa kazi, wachaguliwe kutoka ulayani- kila wilaya ipewe haki sawa-kwa sababu watoto wetu wanaweza kutoka hapa waende walya

ingine, wakienda pale unakuta umemugaramikia nauli ama nyumba ya kukaa, bada ya mahojiano basi anarudi nyumbani bure hajachukuliwa.

Mtoto wa shule akipata mimba shuleni aruhusiwe kuendelea na masomo lakini kwa shule ingine-Hasirudi kwa shule ile kwa sababu wanafunzi wale alikuwa anasoma nao tena amepata mimba amerudi pale italeta picha mbaya. Sheria iliykuwako irudishwe yaani ulipaji wa garama ya mimba nje ya ndoa. Kwa sababu, zamani watoto wetu wakiwekwa mimba shuleni ilikuwa yule ambye amemuweka mimba, anaambiwa agaramikie ile mimba na yule mtoto akizaliwa hadi miaka kumi na nane.

Kuhusu urithi, ni kuwa mwanamke aliyefiwa na mumewe, alindwe na Katiba dhidi ya kurithiwa kwa nguvu, kusumbuliwa na jamaa za mumewe kwa mali alioachiwa na mumewe na kutenganishwa na watoto wake. Kuna wengine wakiwa na waume zao-kama hajarithiwa, basi familia ile wanakuja juu hata kumpokonya watoto mujane yule anabaki peke yake. Mjane akiolewa na mwanamume mwingine, awachie watoto …….wote-kwa sababu kuna wajane wengine wakiachwa, wanakuwa na shida ya kuolewa, wanaolewa na mtu mwingine kando ya familia. Basi, urithi ambao alikuwa amechuma na yule bwana wake, awachie watoto wake kama ataondoka kufuata huyo mme ambaye amemuoa.

Urithi ugawanyiwe watoto sawa bila kuwabagua wa kike au wa kiume. Wazazi wapewe urithi wa mtoto wao aliyefariki-yaani kiwango kidogo; yaani wazazi wa yule mme aliyefariki pia nao wapatiwe percentage ya urithi ule ambao mtoto wao amewacha. Wajane walipwe pesa zao haraka bila kusumbuliwa, kwa ajili ya kuelimisha watoto wao. Tukija katika divorce, mali yote mama alichuma na mumewe, igawe sawa kama wame-divorce. Ndoa yoyote ile ikubaliwe lakini iwe registered kwa ofisi ya Chief. Mali mke aliyo chuma na mumewe, isingiliwe na mke mwingine-pengine huyo mme ataoa mke mwingine, basi mali aliyochuma na mke wake wa kwanza isingiliwe-bali huyo ambaye amemuoa wa pili, watafute mali yao wenyewe.

Mwanamke akitafuta yake mwenyewe andikiwe jina lake kwa sababu, utakuta wanawake wako ndani ya nyumba na waume wao lakini mama ana mali yake na baba ana mali yake- kuna wengine wako pamoja, lakini ile mama ameshatafuta-alitafuta mwenyewe, andikiwe jina lake.

Tukija kwenye biashara, serikali za mtaa ziruhusu biashara ndogo ndogo zifanyike bila ushuru. Ziajiri na kulipa walimu wa Nursery yaani hizi serikali za mtaa. Kuliko wazazi walemeshwe mzigo wa kulipa walimu wa Nursery schools, hizi serikali kama vile tuna Urban Council yetu ya Municipal Council, basi hiyo ichukue jukumu la kulipa walimu wa nursery mishahara.

Tena, hizo hizo serikali ziajiri watu wao wa sehemu za utawala-yaani kama hapa Taveta, wale watakao achiliwo hapa wawe ni watoto wetu wa hapa hapa. Hatutaki soko huru kwa sababu haisaidii. Tukija kwenye maternity, maternity leave iwe ni miezi mitatu. Iwe miezi mitatu ya kupumuzika na(inaudible)basi(inaudible)ya miezi mitatu.

Tukija kwenye mahari, ulipaji wa mahari uwe kati ya maelewano ya aliyeoa na wakwe zake-kijana akikataa achukuliwe hatua.

Tukija kwenye domestic violence, yaani vita vya nyumbani; Hakuna kupiga mme au mke katika maisha ya ndoa; atakayepiga, achukuliwe hatua-mara tumesikia wanawake hupigwa pia waume nao hupigwa wakati mwingine. Basi atakaye fanya hivyo, achukuliwe hatua.

Katika Police station, kuwe kuna officer maalum anayeshugulikia kesi za akina mama ubakaji, vita nyumbani na unyanyasaji. Atakaye mbata mtoto chini ya miaka kumi na nne, afungwe maisha,. Atakaye mwambukizia mtu mwingine magonjwa kwa kusudi, ahukumiwe kifo. Atakaye bata mtoto kwanzia miaka kumi na tano hadi kumi na saba afungwe miaka ishirini.

Walemevu; Walemavu wapewe haki sawa kwa uajiri, urithi, uraia, elimu na matibabu.(inaudible) Tukija kwenye uraia, mwanamke aliye olewa na Mkenya apewe uraia bila malipo, pia mwanamume aliyeo Mkenya apewe uraia-yaani marriage certificate. Ndoa ziwe ni wazi.

Waziri achaguliwe na Wabunge kulingana na ujuzi wake. Tunaenda kumalizia. Kuna kuadhibu; hapa kwenye adhabu tunasema kuwa walimu wa-minimize adhabu kwa wanafunzi kwa sababu utakuta walimu nao, wanapoadhibu wanafunzi shuleni wengine wanawapiga hadi kuwaumiza, huvunjwa mikono ama wengine huwadhibu mpaka wawauei basi, jambo ilo likitokea kwa mwalimu yoyote yule, adhibiwe. Mzazi atakeye ua mtoto kwa kumpiga adhibiwe na Katiba. Yangu ni hayo.

**Com. Domiziano Ratanya:** Nina swali moja hapa Elizabeth- kufafanua tu; Unasema ya kwamba, kama mtu akioa-Mzungu akioa msichana Mkenya unasema ya kwamba hata yeye apewe uraia-awe raia ama hapo sikusikia vizuri?

**Elizabeth Mbele:** Mzungu akija kuoa hapa, mwanamume akija kuoa hapa, asipewe uraia.

**Com. Domiziano Ratanya:** Mwanamume mzungu asipewe uraia?

**Elizabeth Mbele:** Ndio, lakini mwanamke akiolewa hapa basi huyo ni wetu.

**Com. Ratanya:** Okay, tunashukuru sana Elizabeth, tutasoma hayo mandhishi yako katika memorandum vizuri. Na sasa tutaenda kwa John Wambua Muluea.

**John Wambua Muluea:** Asanteni, mimi kwa majina yangu naitwa John Wambua(inaudible)maoni yangu.

Kwanza ningeomba Katiba ambaye tutaandika kwa wakati huu, iandikwe kwa lugha mbili-Kingereza na Kiswahili. Katiba yenyewe iwe ina haki kwa Wakenya wote. Katiba itakayo heshimu mali na haki za watu wote wa Kenya. Viongozi wachaguliwe na wananchi kuanzia mzee wa mtaa na wawe ni wenyeji-mpaka Rais(inaudible). Katiba iwe na nakala ya kuweza kufikia kila Mkenya.

Sheria ziwe juu ya kila mtu. Kuwe na haki kila mtu kurithi mali za ardhi watu(inaudible) Kenya hata mahali mtu anatoka. Vyombo vya habari viwe uhuru kwa kila Mkenya. Rais achaguliwe kwa kura Kenya zima-sio 25% kwa mikoa mune. Ikiwezekana hata iwe 60% kwa kura zote ambazo zitakuwa zina chagua Rais.

Elimu ya msingi iwe ni bure na secondary iwe kwa bei nafuu. Kuwe na vyama viwili vya kisiasa. Vyama vya kisiasa vipewe pesa ya campaign na serikali. Raia halisi wa Kenya wajulikane na hata(inaudible)wawe ni Wakenya. Vyama vya siasa vifanye siasa peke yake. Kuwe na Rais na Makamu wa Rais na Waziri Mkuu. Bunge liwe na uwezo wa kukaa bila kuamurishwa na Rais-pia aliwe na uwezo kujivunvunja wakati unaufaa.

Utawala wa mikoa uwepo na uwezo(inaudible) Wanawake wapewe nafasi sawa za kugombea viti vya uBunge. Kusiwe na Wabunge maalum. Mahakama ziwe na uwezo wa kuanikisha statement na kusikiza case-sio police. Kuwe na Court ya Katiba. Mayor achaguliwe na watu. Sio na madiwani. Mgombea atakaye angushwa kwa asiruhisiwa kuenda kwa chama kingine. Vikundi ambavyo havijasajiliwa, visiruhusiwe kufanya siasa.

Kuwe na lugha mbili za taifa. Mtu ambaye si Mkenya asipewe haki ya kumilikia ardhi.. Mkenya awe na uwezo wa kumilikia ardhi. hata hiyo sehemu anayotokea na(inaudible) Hayo ndio maoni yangu.

**Com. Ratanya:** Okay, asante John Wambua kwa hayo maoni yako. Sasa tuende kwa John Kilelu Mbithi. Are you John kilelu?

**John Kilelo Mbithi:** Kwa jina ni John Kilelu Mbithi, mimi kwa maoni yangu(inaudible) Mwananchi wa kawaida awe na uwezo wa kuandika barua moja kwa moja mpaka kwa Rais ili, mambo haya madogo madogo badala ya kuandika barua kupitia kwa Chief, DO, DC, ama mpaka kwa PC, awe na uwezo wa kuandika barua moja kwa mojo mpaka kwa Rais kama amefanyiwa unyanyasaji.

Kwa vile Kenya kumekua na ujambazi mwingi, tungeomba home guards wawkuweko. Kuhusu soko huru sisi wakulima wadogo sisi hatutaki. Kuhusu majimbo, majimbo haya kama yatakuweko, yatatugawanya kwa misingi ya ukabila. Asanteni.

**Com. Ratanya:** Okay, asante sana kwa hayo machache na ningetaka kuwakumbusha hata wengine, wakati unapeana maoni yako sasa, sikurudia yale yote yamesemwa. Jaribu kusema yale ya muhimu ambayo mi mapya. Kwa hivyo tuendele kwa mwingine, Issac G. Lesing.

**Issac. G. Lesing:** Kwa majina naitwa Issac G. Lesing na mimi ni mkaji wa(inaudible)na ni Mtaveta. Kwa upande wa maoni yangu, naonelea kwamba Katiba iwe ikisikiza maoni ya watu wadogo na wakubwa.

Na jambo linigine tena, ni kuhusiana na mambo ya upande wa maji. Hilo ndilo kubwa. Maji pale(inaudible)lakini kulingana na ile bill ambayo inatokea pale, huwa bill inakuwa juu zaidi. Ni kama tuko sehemu za Mombasa ama Nairobi ama nchi yeyote kubwa. Ninaonelea kwamba Katiba hiyo irekebishwe kwa sababu ni raslimali yetu ya Taveta.

Jambo lingine ni kwamba wale ambao wanaenda kwa-yaani wakishapata retirement, wafikiriwe serikali ipeane malipo yao mapema iwezekanavyo maana wakati mwingine watu wengine huwa waneanda retire, wakishaenda retire, baada ya mwaka mmoja au miwili unakuta yule mtu ameshakufa-na akisha fariki basi inakuwa ni shida, bibi au familia ya yule bwana huwa na shida kupata malipo. Maoni yangu ni hayo.

**Com. Ratanya:** Asante Issac, na sasa tunafika kwa Mary Muroki.

**Mary Muroki:** Kwa jina ni Mary Muroki na sana sana nilikuwa nataka kuongea kuhusu elimu ya wasichana. Kwa kweli wasichana tukiangalia au wanawake, elimu yao iko chini sana zaidi ya wanaume. Ningependelea wanaume na wanawake wote wawe sawa kwa masomo, kikazi-yaani wachukuliwe sawa.

Pili, ni kuhusu elimu ya wakina mama, yaani elimu ya ugumbaro. Kwa kweli hii nayo tukiangalia wamama wengi siku hizi hawajui kusoma, hawajui kuandika-wale wa zamani hawakufundishwa. Pia Katiba iangalie upande huo wa elimu ya watu wazima. Yangu ni hayo tu.(interjection). Yaani serikali iangalie-iandike walimu wa kufundisha hawa watu wazee ili wote wawe sawa, wajue kuandika na kusoma.

**Com. Ratanya:** Okay, asante sana kwa hayo maoni Mary na sasa tutaenda kwa Norman Ochola Daniel.

**Norman Ocholo Daniel:** Jina langu naitwa Norman Daniel na mimi ni mkaaji wa sehemu ya Chale. Maoni yangu niliyo nayo, ni kwa habari ya Chief. Akichaguliwa, achaguliwe Chifu wa sehemu hii ya Taveta kwa sababu yeye ndiye anajua shida ya wanachama ama watu walioko katika sehemu ya Taveta. Na Mbunge akichaguliwa, achaguliwe Mbunge anayejua shida za Taveta; kwa sababu ikiwa patachaguliwa Mbunge ambaye hajui shida za Taveta, tunaona Taveta itazidi kufadhaika zaidi. Tena, nikikumbuka katika hawa watoto ambao- hawa machokora vile wanavyoisha katika sehemu hii au sehemu ya Kenya ni vile hawana baba zao. Na ikiwa walikuwa na baba zao, hawa watoto wangefaidika zaidi. Tungeomba jambo hili liangaliwe sana kwa sababu linazidi kuendelea katika hawa watoto. Na tena jambo linigne ni kama sehemu hii ya Taveta vile ilivyo. Imekuwa na shida sasa zaidi kwa sababu ilikuwa-ilirudi kuwa ndogo kwa hali ya ufanishi ilivyo sasa, watoto hawa wanazaliwa sasa, haijulikani wazazi watawapeleka wapi. Kwa sababu sehemu imekuwa ndogo. Kwa habari ya sehemu hii ya Taveta- yangu ni kama hayo.

**Com. Ratanya:** Unasema imekuwa ndogo, sasa unapendekeza nini?

**Norman Ochola Daniel:** Napendekeza kwamba hii nchi-unajua wale watu waliotuvamia, waonekane kwamba itapangwa namna gani kama nikupunguzwa wapugunzwe kwa sababu sehemu walikutoka, walitoka nchi yao au sehemu yao.

Lakini sasa watoto ambao wako sasa nina hakika kabisa tutakuwa na shida-----Wanaweza kupangia kwa mpango kwa sababu, ikiwa kwamba wale waliokuja lazima wajulikane kwamba wametoka katika sehemu gani na kama kwao kuna nafasi, warudishwe serikali inawajua.

**Com. Ratanya:** Okay, asante Norman na hapo tuende kwa Joseph Lepuku Makiata-unajua haya majina mengine ni mapya. (Laughter).

**Joseph Lepuku Makiata:** Asanteni sana, kwa majina naitwa Joseph Lepuku Makiata. Kuhusu maoni yangu tuu ya Katiba, ningeomba Katiba iangalie hasa kuhusu Ubunge na Udiwani.

Ningeomba katika uchaguzi wa kuchagua Mbunge, pamoja na Diwani, wawe ni wa eneo hilo huyo apewe kikao mbele katika uchaguzi wake Ya pili, ni kuhusu ardhi na mali ya asili. Kuhusu ardhi na mali ya asili ningeliomba Katiba iangalie kuwa katika ugawanyaji ya ardhi hasa sehemu ya Taveta, wapewe nafasi wazee wetu wa Njama waweze kupatiana ardhi kwa wenyeji. Asanteni sana yangu ni hayo machache.

**Com. Ratanya:** Okay, asante Bwana Lepuku Makiata na sasa tunaenda kwa Matthews Savingo.

**Mathews Savingo Mutawa:** Majina yangu ni Mathews Savingo Mutawa, nina maoni machache kuhusu Katiba. Mimi, ningependelea-upande wa utawala, ningependelea Rais asiwe wa chama chochote na pia achaguliwe na wananchi kwa siku tafauti na ile ya Wabunge na awe amepita kwa asilimia hamsini kuenda mbele.

Upande wa police; police wa utawala kama vile AP, police hawa wa kawaida-wawekwe kwa Mkubwa mmoja wasigawanyishwe hiyo ni kuharibu pesa.

**Com. Ratanya:** Wawekwe pamoja?

**Mathews Savingo Muawa:** Wawe under one Commissioner. Upande wa Ubunge; Ubunge wa eneo lolote lile kama tunavyojua, kuna makabila arubaini na mawili Kenya, yaweze kuwakilishwa Bungeni-isiwe kuna makabila madogo "yanamezwa" na yale makubwa. Na ikiwa "yatamezwa" wale nominated MP's watoke kwa hizo kabila ndogo ambazo zitakuwa hazijawakilishwa na wawe wazaliwa na wenyeji wa sehemu watakayo gombea Ubunge.

Upande wa shule-elimu, shule za msingi ziwe bure na iwe ni lazima watoto wote wapelekwe shule. Security; Serikali, Katiba ningeomba kama ingewezekana ipitishe, wafanyi bisahara waweze kupewa-wapunguze ile nafasi ya kupatia watu bundiki ama security yao waweze kupewa wafanya biashara wapewe bunduki za kuwalinda.

Na upande wa serikali, ningependa iwe ya majimbo. Jambo la mwisho, ile vagrant Act irudishwe kama zamani. Asanteni.

**Com. Ratanya:** Okay Mathews, na sasa tunaenda kwa Handol Omondi, yuko karibu? Kama hayuko tutaendelea kwa mwingine anaitwa Othniel Munene. Okay, Bwana Othoniel Munene ambaye ni Chairman wa hii kamiti ya hapa ndiye anaendele sasa. Mheshimiwa endelea.

**Othoniel John Munene:** Jina ni kama mulivyosikia, Otheniel John Munene. Yangu nime andika nitaguzia pia(inaudible) Utengamano na umoja (national integration and unity). Ili taifa liwe taifa kweli kweli, ambalo limeshikana sawa sawa, Katiba inayokuja lazima kuwe vipengele vya kusema kwamba kila kabila lipewe haki sawa na lile lingine kwa kila jambo-kwa elimu kwa uongozi-haki zote ziwe sawa. Paziwe kuna kabila kubwa na ndogo wakati haki hizi zina peanwa. Jambo la pili, ninapitia juu juu tu, ni mamabo ya vyama vya siasa. Kuwe na vyama ambavyo havita zidi vitatu Kenya hii itapunguza mambo ambayo yana ukabila mwingi ndani-katika vyama vilivyoko sasa.

Jambo la tatu; wakati vyama hivyo vinateua wagombia viti, iwekwe siku moja kwa vyama vyote. Hiyo itazuia wale wanayoanguka-wanakosa kula kwa vyama vyao, kuhamia vyama vingine na ku chafua uchaguzi.

Jambo linigine ni mambo haya ya wanyama wa porini yaani National Park. Hawa wanyama kwa vile wametengewa sehemu yao, basi wahakikishe wanakaa huko tu-ikiwa mnyama hasa atatoka kule kwake, aende huko kwa wanadamu basi huyo mnyama awe mali ya wanadamu siku hiyo. Kama ni mnyama ambaye ana-tuseme mali fulani kama pembe, ngozi za thamani basi hizo zirudishwe kwa serekali lakini nyama wajishindie wenyewe.

Jambo linigine, ni hizi kuraupigaji kura; Ili kupunguza mambo ya makesi ya kura, kura zikisha pigwa zihesabiwe pale pale kwenye hicho kituo, halafu jumla yake ndio ipelekwe ikaunganishwe na hesabu ya kura kutoka vituo vingine na yule Returning Officer na atangaze aliyeshinda. Hii Katiba tunayotengeza ni Katiba ambayo tunataka idumu kwa miaka mingi kwa visazi vingi. Kwa hivyo ili Kenya badaye iweze kuwa na umoja wa kitaifa ki-kweli kweli, mambo ya ukabila ukabila yaishe kwa miaka ijayo, ni lazima watu waanze kuishi pamoja na kuheshimiana. Kwa hivyo kutengwe sehemu ya majaribio sehemu hata kama ni huko kwenye National Park, au mahali popote, ambako kutafanywa settlement scheme-mahali popote Kenya, kwenye ardhi ya kutosha na maji ya kutosha watu wa makabila yote wapelekwe huko wahishi pamoja ili watu wajue jinsi ya kuishi pamoja na kuheshimiana. Ukabila utakuja kuisha baada ya miaka fulani tukitumia njia hii. Nchi zingine zimefanya----- Wale ambao hawana mashamba na hiyo pia itasaidia kupunguza kule kukosa kazi-unemployment.

Na jambo la mwisho, nafikiri ili nipeane nafasi kwa wengine kwa maana nimeye andika, ni kwamba mambo fulani kama zile haki za msingi na haki za binadamu , kila mtu ajue haki zake. Askari, Police asianze kunyanyasa watu na kuingia mjini, vijijini kushika watu na ku-search mahali ya watu bila warrant kutoka kortin. Shule za primary ziwe free kabisa na pia, kwenye shule hizo kuwe na vile vifaa ambazo zinaweza kutumiwa na wale ambao ni walemavu-wasitengwe na shule zao special-wawe wanaenda shule na watoto wenzao. Kama ni zile za kusoma kwa mkono-braille, iwe kwa kila shule. Na walimu wale ambao wanajua kufundisha na kuongea kwa kutumia ishara za mkono kwa wale ambao wana ulemavu wa kutosikia waajiriwe kwenye shule-kama primary zote. Hiyo itasaidia sana. Kwa maana wakati mwingine mwanafunzi ana-fail mtihani, kumbe ana hakili lakini hasikii vile mwalimu anasema.

Sasa upande wa serikali-muundo wa serikali, tuwe na serikali ambayo ni ya kibunge sio ya ki-Rais-serikali ya kiBunge ni ile ambayo tutakuwa na Prime Minster-Waziri Mkuu halafu yeye awe na uwezo wake, pamoja na Rais ambaye atakuwa na uwezo uliopunguzwa-sio kama sasa ambapo Rais anafanya mambo yote anakuwa kama Mfalme.

Jambo la mwisho, ni kuhusu usalama wa wananchi na mali zao. Siku hizi Kenya hii, watu hawalali-kupata usingizi kwa sababu ya uhalifu; mtu ako kwake lakini analala na wasi wasi, sasa ili kupunguza uhalifu wale wazee wa mtaa, kwanza wachaguliwe na wananchi wenyewe, halafu kila mtu ambaye atatembelea sehemu hiyo amuone; kama amenda kwa mtu rafiki na atalala hapo lazima mwenye huyo mwenyeji wake amuone huyo mzee wa mtaa na amueleze “kwangu leo nina mgeni na atakaa siku kadhaa”. Mtu yeyote atakaye tubutu ambaye hana mwenyeji, hana huyo ashikwe apelekwe mahakamani aondelewe (inaudible)hapo pengine watu wata kuwa na nafuu kidogo. Kwa hayo machache memorandum nitapeana. Asante.

**Com. Ratanya:** Okay, asante sana Bwana Chairman kwa hayo machache, ambayo ni mengi kidogo na upeane memorandum. Na sasa, huyu Adol Omondi amekuja? Kwa hivyo Adol Omondi hayuko nitaita hapo Fredrick Ndunda.

**Fredrick Ndunda:** Mimi kwa jina naitwa Fredrick Ndunda mkaajii wa hapa Chale. Mimi katika maoni yangu ningependelea majimbo. (end of tape)--- Kwani hapo mbeleni tulikuwa tunaishi hapa. Taveta hii kulikuwako hakuna fujo yoyote. Istahili kwa wakati huu(inaudible)pia ningeliomba ya kwamba serikali ya kienyeiji irudi-iwe pale ambapo(inaudible)

**Com. Ratanya:** Okay, asante sana kwa hayo mafupi kabisa huyu Bwana Fredrick, andikisha majina yako hapo na tuende kwa Josephat Leshamta.

**Joseph Leshamta:** Kwa majina naitwa Josephat Leshamta. Maoni yangu ni kwamba Rais asiwe juu ya sheria na pia achaguliwe na wananchi wote pia kuwe na muundo wa kisiasa wa Rais na Makamu wake na Waziri Mkuu ambaye ndie atakaye ongoza Bunge.

Rais, ningependelea awe Amri-Jeshi-Mukuu kwa ajili ya kuzuia mizozo mibaya kama mapinduzi. Ningependelea wajumbe watakao chaguliwa wawe wenyeji halisi wa eneo ambalo wanalo wanagombania. Kusiwe na mtu mwingine mgeni kutoka kwa jimbo lingine anakuja kugombania katikati sehemu za watu wengine-hiyo inaleta mgogoro na michafuko ya kisiasa.

Uchaguzi uwe wa wenyeji pekee. Ningependelea tena hata wale ambao wanaenda kupiga kura wawe pia ni wenyeji wa zile sehemu kwa sababu, huwa tunaona kwamba kuna transfer za watu kutoka sehemu zingine kuja kuchafua sisasa za sehemu zingine. Ningependelea katika uraia mtu yoyote aliyezaliwa katika sehemu yoyote katika Kenya na ni mwenyeji wa kenya awe ni raia halisi. Pia mwanamke yoyote aliye olewa na mwenyeji wa Kenya kwa ndoa- kwa stakabadhi ya ndoa, apewe moja kwa moja uraia wa Kenya-kwa sababu tumeona sehemu zingine katika Kenya, ni mpakani ambapo watu wanaishi wengine ni kilometer moja kutoka kwa mpaka wanacheza pamoja, wanaishi pamoja wanapendana; sasa nigependelea wapewe uraia moja kwa moja bila maswali mengi-kwa sababu ya ile haki ya ndoa.

Nikija kwa ardhi, iwe ardhi ni ya wenyeji halis wa sehemu hiyo ambayo wanatoka au eneo hilo kusiwe kuna watu wengine ambao wanakuja kuvamia wengine, kuchukua ardhi yao. Nikija kwa mboga za wanyama wa pori, ni muhimu wenyeji wapate faida kubwa katika mapatio yatakayo patikana katika mbog za wanyama wa pori.

Lingine ni, Katiba ihakikishe kwamba wanachama wa vyoma vya kisiasa, wasiwe kama popo-yaani wasiruhusiwe kutoka chama kingine kuenda kingine ovyo ovyo. Kwa hivyo, mimi nigependelea kwamba wale ambao ni wanachama, kuwe kuna uchaguzi wa vyama kwa siku moja ili kuzuia watu kutangatanga. Ningependelea sereikali hii iwe ina muundo pia wa kimajimbo ili katika economy ya nchi, kuwe wale ambao wanaweza kufanya maendeleo katika sehemu zao ama katika jimbo lao waweze kufanya maendeleo-hata kama watazidi zile sehemu zingine-lakini kuwe kuna sehemu fulani inaenda kwa Central Government ama Serikali Kuu.

Mimi ningependa Katiba hii iruhusu mahakama ya kienyeji au zile sheria za kimila, zike fanye kazi kwa makosa madogo madogo, kama vile vita za nyumbani, vita za watoto na ya wazee wao na kadhalika. Kwanza waanzie hapo kabla hawajaingia mahakamani. Na kila kabila liwe na haki ya eneo lao lisiwe ya haki la eneo la mwingine(inaudible).

**Com. Ratanya:** Una meorandum ama huna?

**Joseph Leshamta:** Sina isipokua tu ni point . (interjection—told to sum up)Sasa niko karibu.

Kusiwe na uhuru kuwa kuabudu, isipokuwa kwa ruhusa ya wenyeji halisi wa hapo. Viongozi au wazee waliochaguliwa kimila, wapewe nguvu na uwezo wa kuamua maswala ya ardhi na maswala ya usalama wa nchi katika yale maeneo. Wafanyakazi wa serikali wafanye katika eneo leo lao la nyumubani ili wasije kuwa masikini na vile vile kwa sababu wanajua shida za ile sehemu,

wanaweza kuitatua vizuri zaidi. Na wafungwa wa makosa madogo madogo wawe wanafanyia kazi katika zile sehemu za umma kama mashule, mahospitali na (inaudible) Yangu ni hayo. Asanteni.

**Com. Prof. Idha Salim:** Umesema kwamba kusiwe na uhuru wa dini-ungeweza kufafanua zaidi, kwa nini kusiwe na uhuru wa dini?

**Josephat Leshamta:** Kwa sababu siku hizi watu wengine wanaleta(inaudible)wakitoka mbali ambazo(inaudible)

**Com. Idha Salim:** Yaani ni general worshiping peke yake ambayo unapinga au kuna dini zingine ambayo unapinga pia(inaudible)

**Joseph Leshamta: (**He answers but his answer is inaudible)

**Com. Idha Salim:** Yaani wapendelea dini za kienyeji tu peke yake na hiyo dini tuseme kama Hinduism ikiwapo, mabaniani wasiwe na haki ya kuabudu? Na ikiwa ni wananchi?(answer inaudible) Pia unasema kwamba wananchi au citizenship upewe mke wa Mkenya?

**Josephat Leshamta:** Katika mila za Mwafrika mwanaume ndiye anaoa. Sasa kama mwamamume ameoa mwanamke kutoka sehemu ya Tanzania ama Uganda kwa ndoa takatifu ama ndoa ya serikali apewe uraia…….

**Com. Idha Salim:** Na ikiwa ni mwamamke Mkenya hawezi kumuoa mtu wa nje na yule mume akepewa pia uananchi?

**Josephat Leshamta:** Kwa maoni yangu, kwa sababu(inaudible) wanawake hawaoi wanaume mimi sioni kwamba ni ya maana. Asante.

**Com. Prof. Idha Salim:** Yaani hapa huamini kwamba kila Mkenya ana haki zake sawa na mwenzake akiwa wa kike au wa kiume?

**Josephat Leshamta:** Wanatakiwa wawe na haki zao(inaudible)

**Com. Prof. Idha Salim:** Moani yako, asante.

**Com. Domiziano Ratanya:** Hapo ningependa kupata kitu kidogo tu. Kwa upande wa dini, unasema lazima ikubaliwe na mwananchi. Kama ya Hindi, ni kama hii ya zamani kama ya Catholic ama zingine? Wananchi wakikataa, sasa ungesema aje hapo kwa maoni yako?

**Josephat Leshamta:** Kama wananchi wamekataa(inaudible)utajua pia kwa maoni ya wananchi kwa njia gani(inaudible) unajua kwenda kwa wananchi wenyewe hawawezi (inaudible)maoni yapelekwe kwanza kwa panel of elders halafu wale(inaudible).

**Com. Ratanya:** Na hii panel of elders ni ile ile mnaita Njama ama ni wengine wamechaguliwa kwa njia nyingine?

**Josephat Leshamta:** Kwa hapa kwetu ni Njama ndio yetu hapa kwetu(inaudible)

**Com. Ratanya:** Okay, asante sana huyu alikuwa Bwana Josephat; uandikishe pale. Wewe ni Josephat? Okay asante, tuende kwa mwingine Julius Mekwenchi. Wapi Julius? Okay.

**Julius Mekwenchi:** Asanteni sana ma-Commissioner wetu. Kwa jina langu naitwa Julius Mwanzia Mekwenchi-Mtaveta kuzaliwa na kukulia. Sina mengi mimi ya kuweza kuzungumzia; Hapa kwetu Taveta, hii Katiba ambayo iko sasa hivi, imenyanganya serikali yetu ambao ilikuwa na mamlaka makubwa ambayo inaitwa Njama. Hiyo Njama ni wazee waliokuwa wanateuliwa kutoka kila pembe ya Taveta wanaketi kwa pamoja wanapitisha kila kitu-wanalinda kila kitu ukubwa hata unyonge; mpaka rasilmali zote. Hata wanawake waliolewa wakinyanyaswa walikuwa wanalindwa na hiyo serikali ya wazee. Kwa hivyo, mimi katika maoni yangu naona hiyo serikali yetu ya Njama irudishwe, ipewe nguvu kabisa iweze kulinda mwenyeji wake wa Taveta kuliko kuchukuliwa ma-case madogo madogo ambayo yalikua yanaweza kupitia kwa hawa wazee, inapelekwa mahakamani ambayo inachelewa.

Lingine; mimi nafikiri kila Mkenya nafikiri alijumulishwa kuwa na haki. Sisi Wataveta ni watu ambaoni kabila ndogo.

Hata tukijikakamua nama gani, tunaona bado tunamezwa katika mambo mengi ya siasa- tunamezwa. Kwa hivyo tungeomba Katiba ilioko imulinde-ilinde hili kabila ndogo ambalo ni Mtaveta. Tumejaribu kuweka makabila mbali mbali wanatoroka-wanatuwacha hapa. Tukimchagua huyu, anatoroka anatuwacha hapa sasa tunakuwa kama hatuna uongozi-hatuna kiongozi. Hiyo ndio maoni yangu kwamba, kutoka Mbunge, kutoka Diwani, Chief mpaka na wazee wa mtaa wawe wakipitia kwa hilo baraza letu la wazee wa Njama waidhinishwe basi ndio waendelee. Mimi yangu ni hayo machache tu.

**Com. Domiziano Ratanya:** Nina swali hapa Bwana Julius; Unasema hii serikali ya Njama ambayo ilikuwa zamani-irudi? Ipewe mamlaka?

**Julius Mekwenchi:** Ndio, ipewe mamlaka.

**Com. Domizano Ratanya:** Hapo unataka watawale kwa kiwango gani; kwa sababu kuna President na kuna wengine kama hawa wanapendekezwa, na Ma-Ministers na ma MP; Sasa Njama unataka waingie kwa kiwango gani? Kama serikali kwa

sababu unasema hata wao ni serikali.

**Julius Mekwenchi:** Mimi ninasema kutoka kwa UBunge, ma-Chief na wazee wa mtaa wawe ni wenyeji wa pale, wanachaguliwa ni lile baraza la Njama, ili wajue kwamba wanan guvu ya kuweza kutusaidia sisi Wataveta. Wakikataliwa na lilo Bunge-hiyo serikali ya Njama basi. Upande wa majimbo, mimi ningependekeza majimbo yawepo.

**Com. Domizano Ratanya:** Okay, asante kwa hayo maoni yako Bwana Julius, tumeyasikia sawa sawa na tungetaka sasa kwenda kwa Wilfred R. Leshamta.

**Wilfred Rama Leshamta:** Mimi kwa majina ni kama mliyo sikia, naitwa Wilfred Rama Leshamta. Mimi nina maoni madogo katika mambo ya Katiba. Nilikuwa naomba kwamba katika Katiba yetu wale wanaohusika na kutengeneza wards katika Local Authorities, ziwe zinakubaliana na location-isitoke nje ya Location. Ikiwa ni Location, ndio iwe wazi lakini ward isitoke nje. Vile vile katika mambo ya Local Authority, ushuru ambao unapatikana katika ile ward, huduma itolewe na Local Authority katika hiyo ward na kama hawawezi kutoa hiyo uduma, then wasichukue ushuru. Katiba ni chombo muhimu sana; na Katiba hatuwezi kuwa tunaibadilisha kama nguo-kwa hivyo Katiba ikitengenezwa, iwe inaweza kudumu kwa miaka ishirini ndipo ifanyiwe marekibisho; Lakini isiwe kila wakati Wabunge wakikutana ni kufanya marekebisho ya Katiba. Ikiwezekana idumu kwa miaka ishirini.

Colleges za serikali, yaani viuo vya serikali; Wakati serikali imechukua wanafunzi katika viuo vyao, ni lazima iwe inajua inaweza ikawajiri. Kwa hivyo wanapo maliza colleges iwe kupata kazi ni automatic isiwe kwamba wamejifunza kazi na wanabaki hawana kazi. Upande wa elimu, ni maoni yangu ya kwamba elimu iwe bure kwanzia nursery mpaka class cha nane na ikiwa bure basi, ni kwamba hata majengo, madawati iwe inahudumiwa na Local Authority ili isiwe ni sababu ya kuambia wazazi watoe hiki ama watoe kile-Local Authorities ziwe zinaweza kuweka vifaa vile vinatakikana katika hizo shule; na elimu iwe ya 8-6-2 isiwe ya 8-4-4(interjection)to Standard eight. Elimu iwe 8-6-2 yani primary iwe miaka minane, secondary iwe Form one to Form four na Form five na six ziwe kama zamani, halafu secondary kuweza(inaudible)kwa miaka miwili na kuchukuwa degree zake.

Land; kuna neno ambalo linaitwa squatter; ukiliangalia kwa dictionary, unaona ni mtu ambaye amechuchumaa na anataka kukimbia. Kwa hivyo, neno la squatter lisiweko- liondolewe, iwe ni watu ambayo ni landless. Serikali iwe inafikiria landless-sio squatter kwa sababu, squatter ni mtu anawacha ardhi yake, anakuja kuvamia ya wengine; lakini landless inaonekana kwamba huyu mtu ikichunguzwa katika Republic hana ardhi popote kwa hivyo huyo ndiye mtu atapewa shamba-especially mashamba ya settlement schemes. Nna hizi settlement schemes zinapotokea katika jamuhuri ya Kenya, kila wilaya iwe inapata share yake.

Kazi; Kazi kwa upande wa serikali, watumishi wa kwenda hadi kiwango cha job group F, wawe ni waakaji wa ile

district-wasitoke nje ya hiyo disrtict Mipaka ya utawala; mipaka ya utawala inapotaka kubadilishwa na zile tume zinazohusika, uamuzi usiwe wao pekee yao bila kuhusisha zile tarafa zinazo husika. Yani ikiwa mpaka wa tarafa fulani, na fulani unaitiji kubadilishwa, basi jambo lile lizungumziwe na viongozi wa zile tarafa. Tukiangalia mipaka yetu ile iliwachwa na Mkoloni na ile ambayo iko sasa, zina question mark kubwa sana. Wananchi hawajui ime kuwa vipi na ikawa vipi.

Aina ya serikali; aina ya serikali ni maoni yangu ya kwamba, kuwe na Mzee wa mtaa katika utawala, naibu wa Chief, Chief, DO na DC. Hao DO na DC, wawe ni watumishi wa serikali wanaoteuliwa direct katika kazi zao, lakini naibu wa Chief na Chief, wananchi wa sehemu ile ama hilo tarafa inyaahusika, wapewe mamlaka ya kuwachagua kwa kura ya siri watu watatu, ndio majina yapelekwe kwa serikali, serikali ikachukue jina moja pale. Assistant Chiefs and Chiefs, iwe kwamba wananchi wanachagua kwa kura ya siri, majina matatu wapeleke serikali-na kama mumesikia nimesema DO na DC-sikusema PC. Kwa hivyo PC katika Kenya wawe ma-Governor-wawe ma-Governor ambao ndio watakuwa wanateua wafanyakazi kama ma-Chief katika lilo eneo lao.

**Com. Domizano Ratanya:** Na hao wachaguliwe na nani hao ma-PC?

**Wilfred Rama Leshamta:** PC na DC watachaguliwa na Rais-pamoja. DO awe ni mtu ametoka katika course yake anachaguliwa na ile wizara inayohusika. Lakini DC na Governor, wawe wanachaguliwa na Rais wa nchi. Bunge; Wabunge wawe na miaka thalathini mpaka sabini na tano-umri wao uwe miaka thalathini mpaka sabini na tano. Wabunge wasiwe wakijipangia mishahara; wawe kama wafanyikazi-hakuna mtu anaweza kuingia kazini na ajipangie mshahara mwenyewe. Kwa hivyo mshahara ule wa Wabunge, uwe kwamba unakuwa ni mshahara kutoka Parliamentary Service Commission, ipange hali yao ya mshahara-lakini wasijipangie wenyewe wala wasiwe na Commission ya Wabunge peke yao. Kusiwe na Commission kama ile iliyoko sasa, isiwe ya Wabunge peke yao. Iwe hiyo Commission ni ile ya serikali na inapanga kesi zao.

Rais awe wa umri ya miaka thalathini na tano mpaka sabini na tano na apate kura, three quarter ya quota ya mikoa ama majimbo yalioko Kenya.(interjection) Nimesema ya kwamba Rais apate three quarter ya kura ya mikoa. Kama mikoa ni minane, basi apate kura kutoka mikoa three quarter ya hiyo mikoa. Isiwe tu kwamba ni mkoa mmoja tu umechagua maana mkoa mwingine unaweza kuwa na watu wengi kuliko wengine. Kwa hivyo Rais iangaliwe kimukoa alivyopata kura. Kama si hivyo kura itakuwa ikirudiwa (interjection)ni zote-yaani vile ilikuwa kama (inaudible)ni nane, tukipata kwamba three quarter ya hiyo mikoa ni sita, then awe anapita provinces sita. Sijui kama hapo nimeleweka?

Kila mkoa awe amepita over 51%-isiwe chini ya hapo. Local Government; Councillors wasijipangie mshahara. Councilors wasiwe wakichukua loan katika pesa zetu ambazo zinapatikana katika hiyo Local Authority. Wakitaka loan, wa-apply kama raia wanavyo-apply katika bank-lakini wasijilipe loan.(interjection) Mshahara wao utakuwa umepangwa kwa scale na serikali kwamba councillor atakuwa anapata kiwango fulani cha mshahara; kwa hivyo aishi kwa mshahara wake. Mayor na ma-Chairmen wawe wakichaguliwa kwa kura. Mtu yoyote ambaye ni Mayor, ama ni Chairman, awe anachaguliwa kwa kura.

Mali ya asili; mali ya asili, two thirds ya mali ya asili, ibaki katika ile wilaya ama mkoa. National Park; mali ya National Park inayopatikana katika National Park, one third ya ile inayopatikana pale ibaki katika ile wilaya.

Wanyama wa pori; wanyama wa pori wakae katika National Park, ndani ya National Park na ikiwa watatoka nje na kuharibu mimea, basi mwenye shamba alipwe kufuatana na jinsi mkuu wa kilimo atasema-garama ya ile chakula alipwe. Kusiwe na kiwango maalum tunafidiwa.. Wanyama wa pori wakiua binadamu nje ya National Park, family yake ilipwe million tatu. Maana hivi sasa wanalipwa elfu thalathini lakini walipwe million tatu.

Upande wa uchaguzi, ningeonelea kwamba uchaguzi uwe siku moja katika Wabunge na Madiwani lakini uchaguzi wa Rais uwe tarehe tafauti. Barabara yoyote katika jamhuri ambayo ni class-A iwe ni lazima iwekwe lami si kwamba pesa zikipatikana; iwe kwamba ikishakuwa hiyo class, ni wajibu wa serikali iweke ile barabara lami.

Maji; maji chemchemi na mito pamoja na kingo za mito, zihaifadhiwe na serikali na kulindwa na serikali. Nafikiri yangu ndio hayo. Asanteni.

**Com. Domizano Ratanya:** Okay, asante Bwana Wilfred. Tutaenda kwa mwingine anayofuata, ni Juma Menevu.

**Juma Menevu:** Kwa majina mimi ni Juma Menevu na Mtaveta natoka (inaudible)location. Kuchangia Katiba na maoni yangu ni kwamba kwanza nataka kusema elimu iwe ya bure kwanzia shule ya msingi na irudi ile system ya zamani ya 7-4-2-3.

Kuhusu hospitali, Wizara ya afya, hospital ziwe zinapea matibabu bure hii ipitishwe na Wabunge Wabunge wetu kwa sababu raia wote wa Kenya hawana pesa zakugaramikia matibabu ya hospitali. Kuhusu Bunge, Mbunge awe amatoka sehemu hiyo na kabila hilo, ambaye (inaudible)kitu na pia afanyiwe interview ya lugha ya kabila hilo.

Maoni yangu kuhusu utawala, ni kurudisha sheria ya Chief's Act Chapter 128(interjection) Utawala; Chief, irudi ile sheria ya 128, irudi ile sheria ya Chief's Act Chapter 128 na iwe na kikufungu cha kurudisha wageni kwao. Ardhi na makao; mashamba yalhakikishwe kwote Kenya, ili wenyeji wa sehemu hiyo wasiwe wakavamiwa na makabila makubwa na kunyanyaswa kwa kila njia ya mashamba kwa kuuimia pesa.

Katiba ikiandikwa tungeomba ipelekwe kwa kila shule ili watoto wadogo wanaposoma wawe wameelwa Katiba kuliko kuwacha Katiba katika Bunge peke yake. Yangu maoni ni hayo, asanteni.

**Com. Domiziano Ratanya:** Okay Juma, asante kwa hayo machache, na hapo tutaenda kwa Noel Mekingare.

**Noel Mekingare:** Kwa majina ni Noel Mekingare. Kwanza kwa maoni yangu nilivyo ona ni mambo ya chama(inaudible) pia ningependa katika mtoto wa kike na wa kiume naomba kuweko usawa kama pengine ni wakike, hajakuwa amepotea bwana. Ya tatu, utawala; iwekwe Chief na sub-Chief awe ni mzaliwa na mwenyeji wa sehemu hiyo. Pia katika utawala, kuna huyu Chief na sub-Chief; Unakuta Chief anapata mshahara, sub-Chief anapata mushahara na kuna huyu village elder-mzee wa mtaa anafanya kazi ngumu na halipwi chochote hii ingewekwa kwa Katiba wapatiwe haki yao. Asanteni.

**Com. Domiziano Ratanya:** Okay asante Noel; sasa tutaenda kwa huyu Agustino Nguruwi.(interjection) Peleka pale na uandikishe. Haya, mnakumbuka mbeleni nilisema kama mtu ana memorandum na hataki kuendelea kuongea anaweza tu kupeleka pale iandikwe na atosheke. Na kama anataka kuitetea kidogo, nitampatia nakika mbili. Pia unaweza tu kupeana na unyamaze.

**Alfred Metiaki:** Majina najulikana kama Alfred Metiaki, maoni yangu kuhusu ardhi; Tunavyojua nikwamba ardhi ya Taveta ina asilimia hisani ya watu watatu; Bagizi, Muhoho na National Park Ningependa ya kwamba, wanao miliki ardhi hiyo (interjection) ningependa wamiliki 10% pekeyake ya ardhi hiyo. Na kama itazidi zaidi ya 10% idhini hiyo wapatiwe na community elders-yaani wazee wa njama. Ningependa pia Katiba ilinde mila na desturi na tamaduni za jamii ndogo. Hii ni ya kwamba misitu na maziwa ambako kunafanyiwa tambiko visitumiwe na watu binafsi.

Maji: Ningependa mito na chemchemi zote zisiwe zikitumiwa na mtu binafsi. Kwa mfano, utakuta kuna mfereji mmoja (inaudible)ambao mtu anaweza kukata bila idhini ya serikali ama ya jamii. Ningependa kuwe na mpangilio kutoka kwa jamii kutumia maji hayo.

Tatu, ningependa maji ya Mzima Springs- ambayo ni maji ya Taveta- lakini hainufaishi watu ama jamii ya Taveta, ningependa mapato yote yanayopatikana itolewe 10% ili wafanye maendeleo ya jamii hapa Taveta.

Siasa: Ningependa kuwe na siku moja ya vyama vyote kuteuwa wakilishi wao wa Bunge. Pili, ningependa Katiba ihakikishe ya kwamba ma-Chief na ma-Sub-Chief wamepatiwa bunduki za kuwalinda wananchi. Kwani hivi sasa wananchi hawako katika usalama. Pia ningependa Rais asiwe ana uwezo wa kutoa ama kufungulia wafungwa-yaani Presidential Amnesty. Kwani kufanya hivyo, ndipo hualifu unazidi. Pia ningependa magereza wasiwe wakitoa remission kwa wafungua kwani wanapopatiwa remission hiyo wahatifu hao hawatumii fursa hiyo vizuri. Asanteni.

**Com. Domizano Ratanya** Ok Bwana Wilfred na asante sana kwa hayo machache na sasa tunaenda kwa Peter Gori Ntimiru.

**Peter Gori Ntimiru:** Kwa majina naitwa Peter Gori Ntimiru. Maoni yangu kuhusu Katiba hii mpya tunayo rekebisha sasa, ningependekeza kwanza kuhusu Administration. Wazee wa mitaa wawe wakichaguliwa na wananchi wenyewe. Assistant

Chiefs na Chiefs wawe wakiteuliwa na idala ya utawala. Kama inavyofanyika sasa.

Madiwani: I mean, hapo hapo kwa ma Chiefs, ile sheria yao ya CAP 128, warudishiwe. Kuhusu Madiwani na Wabunge; Uchaguzi wa Diwani au Mbunge anyetaka kuchaguliwa mahali pale awe ni mwenyeji na mzaliwa wa eneo hilo. Recruitment za Police na pia hudumu ya vijana kwa taifa kila kabila lipewe haki sawa na lile kabila lingine.

Baraza la mawaziri: mawaziri wawe wakichaguliwa na Rais mwenyewe, lakini pawe na kifungu kinacho muezesha kuwachagua ki-mikoa. Kila mkoa uwe na mawaziri sawa na mkoa mwingine. Pasiwe na mkoa wenye mawaziri wengi kushinda mwingine.

Upande wa ardhi, ningependelea ardhi-ugawanyaji wa ardhi uhusishwe wazee halisi wa maeneo hayo. Kuhusu shule, nigelipendekeza shule ziwe za bure kuanzia nursery hadi darasa la nane. Ni hayo.

**Com. Ratanya:** Tunashukuru. Kwa sasa ni Eric Muramba. Yuko? Nafasi ni yako.

**Eric Harrison Muramba:** Asante. Kwa majina naitwa Eric Harrison Muramba na maoni yangu ni haya machache. Kwanza nilikuwa na maoni juu ya Mbuga za wanyama. Naona kama kuna ulalamishi mkubwa. Watu wanaona kama wanyama wangechukua sehemu nyingi ya ardhi na wananchi wanalalamika hawana mashamba. Naona ingekuwa ni haki wananchi wahusishwe ili kufua ni eneo gani ipewe wanyama na lipi lipewe wananchi. Lakini kwa sasa kuna hali ya kuona kwamba wanyama wanapendelewa zaidi. Halafu kuhusu mtu kuwa na ardhi, kuna watu ambao wana maelfu ya ma acre ya ardhi wakati wengine hawana ardhi. Naona ingekuwa ni sawa kuwe na kiwango cha juu-yaani kipimo ambacho mtu hawezi kuwa na ardhi kiasi hicho. Kama ni acre mia moja, kama ni acre ngapi lakini-isiwe mtu anaweza kuwa na maelfu ya acre wakati mwingine anatafuta hata nusu acre.

Kuhusu urithi, ni haki kabisa kwamba wanawake wawe na haki ya kurithi mali. Wanawake kwa wanaume wote waweze kurithi mali. Isipokuwa tujaribu tuende njia ambayo haitapendelea upande wowote kwa sababu inawezekana tukitoa usawa hivi hivi bila kuangalia, mwingine hapo atakuwa na haki mbili za urithi. Kwa sababu mtoto wangu wa kike nitarithisha kwangu, halafu ataolewa halafu kule kwa mme wake pia vile vile atadai arithi. Sasa itakuwa hailaweki lakini mwanamke arithi watu alikozaliwa ama alikoolewa. Kwa hiyo kuna haja tu warithishe lakini tuwe na njia ambayo haitapendelea upande mmoja.

Kuhusu mishahara kwa jumla hasa ya Wabunge, si sawa kabisa Wabunge wajipangie mishahara yao. Kuwe na kama ni tume, kama ni-namna ya serikali kupanga mishahara watu wote Kenya. Kama ni Wabunge, kama ni madiwani lakini isiwe kuna kikundi ambacho kinajipangia mishahara yenyewe kwani hiyo hali italeta hali ya kupora pesa za wananchi. Halafu kuna haja ya kuwa na office ya yule mtu wa kupokea malalamishi ya wananchi-yule ambayo kwa kingereza anaitwa Ombusman. Yaani Ombudsman ni officer, ama ni mkuu ambaye ana haki ya kusikiliza vilao za wananchi za kila aina. Kama ni mambo ya ufisadi, kama ni mambo ya utawala jinsi tunavyo endelea-lakini iwe ni offici ambayo inakubali mtu yoyote kuingia na kueleza malalamiko

yake bila kuwa na wasisi kwamba yuko katika hatari ya kukamatwa. Napendekeza kuwe na office ya Ombusman na iweze kupokea malalamishi yale ambayo wananchi hawawezi kuyatoa kwa ma offici mengine-hasa ufisadi-ufisadi hivyo.

Halafu kuhusu Rais, Rais asiwe Mbunge. Kwa sababu Rais anapokuwa Mbunge atajitahidi sana ili achaguliwe tena katika eneo lake la uBunge. Najitihada hiyo. Hasababisha yeye kumwaga pesa nyingi katika eneo lake, ajenge kama ni vitu-yaani vitu vingi-atengeneze pale kwenye eneo lake ili achaguliwe tena Bungeni. Ingekuwa bora yeye awe ni mtu ambaye hawakilishi eneo la uBunge. Na hata vile vile mawaziri wake wanaweza kuwa Wabunge ama wasiwe Wabunge. Hata wale sio Wabunge kuna wengine wako na uwezo wa kuongoza nyadhifa ambazo wana uwezo nazo bila kuwa Wabunge. Mfano wa America nafikiri kama ingekuwa si hivyo tusingepata labda mtu----

**Com. Ratanya:** ….kuwaongoza ali (inaudible) fulani. Halafu, kuhusu majimbo, mimi ningependekeza serikali ya majimbo-isipokuwa isichukuliwe kuwa majimbo ni ukabila. Inaonekana inonekana hiyo ndiyo hali ambayo tunaichukua sana. Tunaposema kuwe na jimbo fulani kwa eneo la Pwani si kwamba ati iwe jimbo la Pwani ni la makabila fulani pekee yake. Uhuru wa kukaa mahali popote Kenya uweko, lakini haya majimbo ni kwa ajili ya kurahishiza utawala-sio kwakutenga makabila fulani-kabila hili, jimbo lao ni hili-hapana. Ni kurahisisha utawala si kwa kueneza ukabila.

Nita maliza kuhusiana na walemavu. Nafikiri malalamishi ya walemavu ni mengi sana, yame sikika. ihi Katiba inapaswa izungumuze wazi kwamba walemavu wawe na haki ya kupata kazi sawa na wengine-kazi za aina yeyote ambayo mtu ana ujuzi nazo na anaweza kufanya, apewe bila kuangalia ulemavu wake.

Halafu, katika usafiri vile vile walemavu wanateseka sana hat vile tunavyoingia katika matatu, unaona mlemavu ana taabu ya kupanda kule na hata akingia gari kule kunakuwa kuna taabu. Kwa hivyo sijui kama kuna namna labda hizi gari ziundwe katika hali ya kuwa kuna eneo ambalo mlemavu anaweza kuenda akaketi hapo na mti wake-tuseme kama ni mkongojo.

Kwa kumaliza nitasema pia vile vile, kuhusu hawa walemavu ni kwamba kunaweza kuwa kuna interview imeitwa mahali na hii interview iko juu ya gorofa. Halau namna ya yeye kufikia kule juu ya gorofa inakuwa ni vigumu. Kwa hivyo either nyumba zetu zijengwe katika hala ambayo kwamba mlemavu anaweza kufika juu, ama interview ifanywe chini ambapo mlemavu anaweza akafikia. Na kwa hayo machache nimeshukuru.

**Com. Domiziano Ratanya:** Okay, nimesema asantei Eric, peana memorandum yako hapo; Na kwa sababu tunakaribia saa saba hata ingawa naona kama imefika, tutakuwa na break na tutarudi tena saa nane-lakini tungetaka kumaliza hawa-watumie dakika moja moja; huyu Alfred Munene na Thomas Nzali, tukimaliza hawa wawili, tutajitarishe kwenda break kidogo halafu tutarudi tena saa nane kamili. Hebu tuende kwa haraka kwa Alfred Munene-dakika yake na halafu Thomas ajitayarishe. Alfred Munene, inaonekana Alfred hayuko, na Thomas Nzau?

Hata Thomas Nzau hayuko.  Kwa hivyo wananchi sasa tumekubaliana tuende break mupate lunch haraka haraka ili tuweze kurudi saa nane.  Asanteni sana.

**Com. Domiziano Ratanya:** Julius Kimondo.

**Benson:** Kwa majina naitwa Benson (inaudible) Kuna hawa tunaweza kuwaita chokora, naomba serikali (inaudible)kwa sababu wanapata shida (inaudible)wazazi wao wachunguzwe kama wapo au wamekufa kwa sababu ikiwa wako hai (inaudible)wanapata shida nyumbani.  Tukija kwa upande wa kina mama (inaudible) voters; Serikali ijaribu kuangalia shida za akina mama pia (inaudible) ili waweze kupiga kura ambazo (inaudible)ardhi pia ina(inaudible)  Kwanza….pia tuna shida. (inadudible)

Naomba pia serikali (inaudible) shule kwa sababu kuna shida.  Fees imekuwa(inaudible)

**Com. Domiziano Ratanya:** Tutaenda kwa Julius.  Julius hayuko karibu, tutaenda kwa Alfred Mwakange, Saleh Misila. Endelea Saleh.

**Saleh Misila: (inaudible)**shida ya ngombe ukienda kununua (inaudible)wakati tulikuwa na wazungu, walikuwa wakituruhusu (inaudible) hiyo kitu Katiba iangalie.

Kuna shida ingine ni ya ugonjwa.  Ukienda hospitali unambiwa hakuna madawa na dawa iko.  Sasa hii dawa ya serikali kwa nini watu wanauziwa?  Kukiwa pesa mtu ananunua dawa kama huna pesa unambiwa dawa hakuna.(inaudible)

Kuna mambo ingine Katiba, (inaudible) barabara zimekuwa mbaya magari hakuna unakuta ni kwa sababu barabara ni mbaya. Muangalie kama hii barabara itatengenezwa namna gani.  Wakati wa ukoloni barabara zilikuwa nzuri.  Wale watu ambao ni wa barabara hawatengenezi na wanzlipwa mshahara na barabara zimekua mbovu.  Magari yananguka ovyo ovyo kwa ajli njia ni mbaya.

Kitu kingine ni mjue kuna watu maskini na matajiri.  Watoto walioko nyumbani wamekosa pesa ya kusoma niwengi-wamekosa wazazi(inaudible)kwa ajili ya kukosa pesa.  Kwa nini serikali isiteremshe pesa ziwe kidogo ndio watoto wote wasome?  Mtoto mmoja analipiwa elfu kumi-na huyo ni ntoto mmoja-kuna wengine.  Kulipia watoto wote na wewe huna kazi unafanya-umekaa nyumbani tu.(interjection)

Nataka kupendekeza fees iwe ndogo, maana hata kupeleka mtoto nursery, ni shillingi elfu kumi.  Haya ukitaka kupeleka mtoto darasa ya kwanza ni shillingi elfu kumi(inaudible)na mwenye kulipa  ni mmoja na hana kazi (inaudible)  hiyo kitu inatuma sisi wazee na tombee hapa tuwe tunachunga ngombe hapa.  Wakati wa mkoloni tulikuwa tanaruhusiwa---(inaudible)

Kuchunga majani ikiwa (inaudible) (interjection) shamba ni lake lakini ame lima huko pengine ameacha (inaudible) na yule ngombe anakunyanganya na shamba (inaudible)hata wanapigwa risasi.(inaudible) anachija anauza nyama ile pesa ni yake(inaudible)
Hilo jambo mwangalie sana. (inaudible)

Ya mwisho, hapa hatujapata land (inaudible)mashamba yetu. Mashamba yetu tunaomba land (inaudible) hiyo mashamba sio yetu ni pori ya wanyama na wanyama hakuna (inaudible)

Lakini kuna neno lingine nimesahau. Hapa tuna chama chetu hapa kinaitwa Society (inaudible)na DO anajua hii report na Chief anajua hii report (inaudible)

**Com. Domiziano Ratanya:** Okay Mzee Msilah tunashukuru kwa hayo maoni yako asante. Na kwa sasa tutaenda kwa Richard M. Leshamta. Richard yuko? Christopher Metaiso, Christopher yuko?

**Christopher Metaiso:** Mimi kwa jina naitwa Christopher Metaiso na ni Mtaveta. Katika Katiba ningeomba ya kwamba walimu wa nursery kuwa serikali haiwangalii. Sasa ningeomba katika Katiba iwe ni mojawapo walimu wa nursery serikali itasimamia kuwalipa mshahara.

Ingine ni kuhusu Mbuga za wanyama. Katika Mbuga ya wanyama, ni kwamba kuna pesa ambayo inapatikana ya kigeni katika mbuga hizo za wanyama. Lakini tunaona ya kwamba haisaidii hizi sehemu ambazo hizo mbuga ya wanyama ziko haisaidii wakaaji. Kwa hivyo katika Katiba ninaomba ya kwamba kuwe kunatoka asilimia hamsini iweze kufaidi wakaaji wa eneo hilo la mbuga.

Kuhusu rasilmali kama vile sehemu za maji; ningependekeza katika Katiba kabla labda kama maji kutoka nje la eneo ambalo hilo chem chem iko (inaudible) kutumika kwa sehemu iko. Kwanza kuangaliwe kwanza wale wenyeji wenyewe je, hiyo maji inawatosheleza? Na kama haijawatosheleza basi wao iwe nafasi ya kwanza wao kupata. Na wakati yale maji yanatoka yakienda, katika Katiba kuwe kwamba kuna asilimia fulani itakayokuwa inabaki kwabajili ya kusaidia eneo hilo.

Katika hali ya uchaguzi ningependa kwa Katiba kuwe na kipengele ambacho kitaruhusu ya kwamba wakaaji, au wenyeji ndio watakao gombea nafasi za kutawala-kuanzia ma-Councillors, Wabunge (inaudible) Katika utawala, wazee wa mitaa wawe wanachaguliwa na wananchi. Isiwe kwamba ni Assistant Chief atawachagua au kuwapendekeza; lakini iwe ni wananchi wanafanya hiyo kazi. Na pia kuhusu ma-Assistant Chief , kuwe kwamba wananchi ndio watakao pendekeza wale watu ambao wanawataka waweze kuwa Assistant Chief na hata ma-Chief, halafu ndipo watume hayo majina yaende mbele ndipoza serikali ipendekeze kama watu tuseme watatu ambao watakgombea (inaudible) serikali itakapo pokea hayo majina, iamue ni yupi

itakaye mchagua.

Na, jambo lingine ni kuhusu rasilmali kama vile tuseme mashamba. Kuna sehemu ambazo zilikuwa hapo tangu wakati ule wa Ukoloni kulikuwa mipaka imewekwa. Lakini tunaona wakati huu kwa sababu Bunge linarekebisha Katiba lenyewe bila wananchi kuhusishwa kuna sehemu zingine zimenyakuliwa zikapelekwa katika mikoa mingine-ambayo ni rasilmali ya sehemu nyingine.
Katika Katiba ningeomba ya kwamba hizo sehemu ambazo zilinyakuliwa ziweze kurudishwa yaani ile mipaka ya zamani irudishwe.

Jambo lingine ni kwamba katika uajiri tuseme recruitment wakati inafanyiwa, ifanyiwe katika location; ifanywe katika location. Na wale watakao chukuliwa wawe ni wenyeji wa sehemu hiyo na kuwe na nafasi sawa wakati wakuchukua-si kwamba kabila fulani wako wengi wawe wanachukuliwe wengi na hapo kwengine wako wachache wanachukuliwa wachache lakini kuwe na nafasi sawa.

Katika kuajiriwa kazi, kuwe pia na nafasi sawa-iwe ni mwanamke, iwe ni mwanamume, nafasi itolewe sawa. Katika kielimu pia kusiwe kunapangiliwa kiwango cha elimu-labda (inaudible) wanawake au pengine masomo ya pangiliwe kwamba mwanamke hastahili kusomea somo hili au mwanaume yeye ndio anastahili. Kusiwe na hali kama hiyo lakini kuwe na usawa.

Jambo lingine ni kwamba katika shule, darasa kwanzia nursery mpaka darasa nane vile ilivyo sasa, ningeomba katika Katiba kuwe na sheria ya kwamba watoto wasome bure-na hii bure ni kwamba mzazi labda agaramikie kununulia mtoto kitabu na kalamu na uniform peke yake. Lakini kitu kama majengo na mambo yoyote mengine yanayohitajika, hatijika iwe kwamba serikali ndio itakayo weza kugaramikia.

La mwisho, mimi ningependekeza ya kwamba katika upande wa Rais, Rais asitoke katika chama chochote achaguliwe na wananchi. Asante.

**Com. Domiziano Ratanya:** Okay, asante sana Bwana Christopher. Mateus yuko? Issac M. Kimboi? Robiana Makingare.

**Robiana Makingare:** Mimi kwa majina ninaitwa Robiana Makingare, mimi natoka (inaudible) location. Kwa maoni yangu ya Katiba-kwa niaba ya waKenya ningeliomba kwamba sereikali iwe ya majimbo. Na serikali hiyo, iwe na Waziri Mkuu na pia kufikia kwa Mikoa kuwe na ma-Governor.(interjection) Majimbo-si mikoa; Majimbo.

Na ningependa kusema-nikiingia kwenye Katiba Waziri Mukuu awe na mamlaka ya kuunda serikali. Kutoka hapo tunakuja kwenye ardhi. Mipaka ambayo ilikuwa imetengwa na waKoloni kutoka mwanzo mwa makabila yaliokutwa-yote arubaini na sita- Katiba isimamie mipaka hiyo irudishwe iliyokuwa.

Tukienda kwa utawala wa chini, tukiingia kwa Ma-Chief pia ma-Chief wapewe ule uwezo ambao walikuwa wamepewa awali na Mkoloni. Hiyo ina maana kwamba hakutakuwa na (inaudible) katika makabila mengine. Tukienda kwenye shule, maoni yangu ningeliomba, kuanzia nursery mpaka darasa la nane, isimamiwe na serikali kwa kila hali. Na kufikia kwenye secondary, pia Katiba iangalie kiwango kinachamwesheza mtu wa kila nafasi aweze kushiriki ili elimu ipatikane kote nchini.

Tukirudi kwenye Bunge, maoni yangu kwa waKenya wote, ningeliomba Katiba isimamie kwamba kila Mbunge anaye omba kiti cha Ubunge kwanza awe ame idhinizwa na wazee wa kabila lile na pia awe ni mzaliwa wa sehemu hiyo na anajua mila na desturi za sehemu hiyo.

Tukija kwenye wanyama, katika Katiba hii ningeliomba kwamba wanyama walioko sasa hivi nchini, kwa vile wana sehemu zao ikiwa watakuja kuharibu mali ya mwananchi au kumdhuru mwananchi ama kumua mwananchi basi mwananchi huyo alipwe ridhao ambayo inaweza kutosheleza kuangalia familia yake kwa maisha yake yote.

**Com. Domiziano Ratanya:** Una maandishi, una barua? Unaweza kupeana. Kuna Reverend Stephen Norman? Reverend yuko karibu? Ngonea R. Mukirimu?

**Ngonea Robert Mukirimu:** Kwa majina mimi naitwa Ngonea Robert Mukirumu na mimi ni mkaaji wa Challa na ni Mtaveta. (inaudible)Katiba ya Kenya ningeomba kwa maoni yangu, kwamba Rais awe anachaguliwa na wananchi na asitoke kwa chama chochote.

Kwa upande wa elimu, ningeomba Katiba ambayo itakua na serikali wakati ujao, ituangalie sana sisi wazazi wa hali ya chini kuhusu elimu kwa sababu, elimu imekuwa ghali mno kwa watu wa hali ya chini. Kuanzia nursery mpaka primary ningeomba Katiba itusimamie itusaidie kwa kutufundishia watoto hasa kutoka nursery mpaka standard eight.

Na kwa habari ya uchaguzie wa Bunge, Wabunge na wa Councillors, Mbunge lazima awe ametoka kwa eneo ambalo anaenda kuombea kiti Bungeni na asiwe ni mgeni wa kuja-pamoja na ma Coucillors-wote wawe wa hapa nchini.

Na kwa upande wa wanyama mwitu ambao ni National Parks, kwa kweli (inaudible) sisi, watu wa hapa ni wakulima na tunategemea kilimo. Na baada ya kulima, wanyama huja sana kutoka kwa National Park, wanakuja kuharibu mimea yetu. Ningeomba Katiba ambayo hakuwa katika serikali iangalie sana jambo hilo la wildlife kwa sababu wanatuharibia sana mimea. Ninatumaini yangu ni hayo.

**Com. Domiziano Ratanya:** Okay, asante Bwana Mukirimu. Kithuka Munyoki, ako karibu?

**Kithuka Munyoki:** Kwa majina ni KithukaMunyoki. Maoni yangu ni kuhusu elimu. Elimu ningelipendelia serikali iangalie mambo ya elimu kuanzia nursery mpaka standard eight-iwe ni bure.

Pili, matibabu serikali iweke bure. Katika uchaguzi ningelipendelea kuwe na uhuru kwa Mkenya kuchaguliwa mahali popote. Nne, wanyama wamekuwa na uwezo mukubwa kuliko wanadamu. Wamekua na maeneo makubwa kuliko watu. Ningelipendelea serikali ijali watu kuliko wanyama. Ni hayo tu.

**Com. Domiziano Ratanya:** Okay, asante Bwana Kithuka kwa hayo machache na kwa hivyo tutaendelea kwa mwingine ambaye anaitwa Julius Nyaki, ako karibu? Okay Julius Nyaki inaonekana hayuko. Charles Kanene? Kama Charles hayuko tutaendelea kwa huyu mwingine ambaye anaitwa Clementina. Clementina yuko? Then tuna Eusta Leshamta-eh nimejua sasa-Leshamta. Eusta Leshamta yuko karibu?

**Eusta Leshamta:** Kwa majina ni hayo mumesikia, mimi ni mkaaji wa hapa Challe, Taveta. Mimi nigependelea mwanamke yoyote awe na urithi-awe na uhaki katika boma ya baba yake sawa na mwanmume.

Pia, ningependelea kama baba ana wanawake wengi wote wawe na haki- awaangalie wote, kama mtoto akiwa ni wake, (inaudible) na aangalie hawa wanawake wote katika uhaki, katika (inaudible) na katika uhaki. Asiwe anangalia upande mmoja.

Kwa upande wa elimu, ningeomba elimu kuanzia nursery mpaka eight iwe bure. Na kwa upande wa mashamba, ningeomba Chief ama wazee wa mtaa waangalie haki ya mnyonge wasiangalie unyanyasi. Mtu akiwa ana kesi asiwe anaangalia yule ako na pesa ndie anaangalia mambo yake. Kuwe kila mtu awe na haki na wazungumze hiyo case ikiwa kwa uhaki, nani ambaye ananyanganya mwenzake wasiwe wanazungumuza kupendelea au kuangalia mambo ya pesa.

**Com. Domiziano Ratanya:** Asante Eusta Leshamta na sasa tutaenda kwa Ndululu Linda, Ndululu yuko? Okay, kama Ndululu hayuko kuna huyu mwingine anaitwa Sukuti Muthongo, Muthongo yuko? Hajaingia? Hebu sikilezeni majina sasa; Kama kuna yeyote ameandikishwa na hakupeana maoni yake. Julius K. Kimondio, amekuja? amepeana makaratasi? Na huyu mwingine Alfred Makange, hata yeye alipeana? All right. Then Richard Leshamta alipeana makaratasi ama haja ingia? Matheaus M. Kamosu? Issac M. Kemboi, hayuko? Tena Reverend Stephen Norman? Julius Nyati? Charles Kanene? Clementina Metuo? Ndululu Linda? Ikuti Muthongo? Rose Milongi? Josephine Mwendwa? Agnes Nyingi? Robin Lesen? Okay kuja kama ni wewe. Endelea.

**Robin Lesen:** Mimi kwa majina ni Robin Lesen, mimi nimezaliwa Challa, Taveta, mimi Mtaveta. Katika maoni yangu ningependelea kuangaliwe katika Katiba ya Kenya kuwa, je, kuna haki mnyama kukula mimea ya mwanadamu? Mimi nauliza kwa nini mnyama ale mimea kwa shamba ya wanadamu? Singependa mnyama ale mimea ya mawanademu. Kama ingewezekana huyo mnyama azuiwe asile mimea hiyo. Akila-serikali iangalie kama itawezekana kuzuiwa.(interjection)

Ingewezekana hiyo mimea iweze kulipwa gharama ya juu.

Ingine ni katika upande wa wakaaji wa Taveta. Sisi wakaaji wa Taveta, wengi wao hawana mashamba. Ingelistahili kuwa wale wengine ambao waliokuja wageni kuchukua mashamba ya wa Taveta, kama wana shamba kubwa kiasi ambapo wale wenyeji hawana shamba hiyo, igawanywe.

Na kuna neno moja, ambalo wanasema-squatters. Hilo neno squatter, sisi Wtaveta tuna- ona ajabu-kuona kwamba sisi Wtaveta wazaliwa wa Taveta tutakuaje ma-squatter? Hatungependelea kuwa ma-squatter-tungependelea sisi ardhi hiyo iwe ni yetu wazaliwa wa Taveta. Bado sija-maliza;

Pia, kuna maji ya kutoka Mzima Springs. Hayo maji ya Mzima Springs ya Taveta, ni wazaliwa wa Taveta. Ni kwa nini maji hayo yatoke hapa Taveta yaende Mombasa? Ningependelea maji hayo yatumikeTaveta-wa Taveta wote watumie maji hayo. Ninaongea neno moja la mwisho kuhusiana na maji hayo; hayo maji ya Mzima Spring. Kama ingewezekana serikali katika Katiba ya Kenya, kutoa pipe pale ya kuweza kunyunyuzia mashamba huku-kwa sababu mashamba mengi hayana maji ya kunyunyzia. Yangu ni hayo, si na mengi.

**Com. Domiziano Ratanya:** Tulikuwa tumeita Reverend Stephen Norman, kama yuko around anaweza kuendelea.

**Rev. Stephen Norman:** Asante, ninashukuru sana. Maoni yangu kwanza nitaanza na power za Rais. Rais power zake zile za kusema ya kwamba ndie atakuwa amri mkuu kwa jeshi la Kenya zipunguzwe-kwa jumla nina sema power za Rais zipunguzwe.

Pili, kuhusiana na Bunge. Tuwe na Bunge mara pili. Bunge la Senate la Bunge ya Wakilishi ambapo tutakuwa na uongozi pia wa Waziri Mkuu. Na hapo hapo, huenda kukawa labda kifo cha Rais kimetokea, Speaker wa Bunge awe na mamlaka ya kushikilia nchi mpaka uchaguzi ufanyike.

Kwa upande wa ardhi, Serikali ama Katiba, isiruhusu ile hali ambayo watu hupewa wakae na mashamba zaidi ya miaka mia moja.

**Com. Domiziano Ratanya: (interjection, inaudible)**

**Rev. Stephen Norman:** Isiwe zaidi ya miaka mia moja-lease, yaani iteremuke kama miaka kumi-mwisho kabisa ni miaka ishirini lease. Na pia umilikaji wa ardhi (interjection) Hiyo lease iondolewe, itupiliwe mbali. Umilikaji wa ardhi; Mtu yeyote asiruhusiwe kumiliki ardhi zaidi ya acre hamsini. Kwa mfano, kama sehemu ya Taveta, sehemu kubwa ya ardhi iko kwa watu wawili. Ni Uhuru, ni Muhoho pamoja na Criticos pamoja na mbuga la Wanyama.

Kuhusu upande wa kuabudu, ama upande wa dini, Serikali kwa mfano, Rais asiwe na mamlaka ya kuchagua kiongozi wa dini. Kwa mfano nikija katika ndugu zetu wa Islam, Kadhi wao mara nyingi Rais ndiye anamchagua, lilo jambo isiruhuswe na liondolewe- waachiwe wenyewe(interjection) Chief Kadhi wao wenyewe.

Kugombea kiti cha Ubunge. Kugombea kiti cha Ubunge, asiruhusiwe mtu kugombea wa kutoka sehemu nyingine. Awe ni mwananchi wa kuzaliwa sehemu ile-maana atakua na uwezo wakuelewa matatizo na kujua shida ya wananchi wa pale. Makabila madogo yapewe pia sauti, yasikike katika (inaudible) (interjection) Kama ni Bunge wahakikishe kwamba wana mwakilishi Bungeni, yaani hivi ni kusema kila kabila ambalo liko Kenya, wapate nafasi ya Mbunge wao katika Bunge. Nimemaliza.

**Com. Domiziano Ratanya:** Stephen enda pale na asante sana Rev. Stephen. Na sasa tunaenda kwa Philomena C. Mushingati. Ameingia?

**Philomena C. Mushingati:** Mimi kwa majina ni kama vile mumesikia, ni mzaliwa wa Kwale lakini nimeolewa Taveta na nimeishi Taveta kabisa.

Kitu ambacho ningesisitiza zaidi ni kuhusu akina Mama. Wakina mama wapate haki zao sawa na wakina baba. At least na wao wawe wanajisikia kuwa wana nafasi katika nchi hii na wasichana wao waweze kulindwa. Kama kwa mfano ubakji wa wasichana uweze kuchukuliwa hatua kali. Vile munavyojua, kuna maradi ya ukimwi ambayo yana adhiri sana maendeleo. Kwa hivyo nilikuwa naomba hiyo iangaliwe zaidi. Mimi sina maneno mengi. Ninashukuru.

**Com. Domiziano Ratanya:** Okay, asante sana Madam Philomena kwa hayo machache na ni machache kabisa ya muhimu. Na tunataka sasa kuenda kwa Nimrod Mutangaoru. Yuko karibu?

**Nimrod Mutangaoru:** Asante sana Bwana Commissioner, mimi nina maswala hapa, pengine ni mengi kidogo lakini nitajaribu kuyapitia kwa ufupi-nikieleza tu yale ambayo ni ya muhimu zaidi.

Nina swala kuhusu Bunge na ningeanza na kule bungeni. Pendekezo langu juu ya kuwachagua ama kupata Wabunge ipasavyo; hapa ningependa tu kuongeza kwamba, mijadala na ya Bunge itangazwe moja kwa moja ili wananchi wapate kusikia wenyewe-kwa masikio yao-isiwe kwamba ni mambo ya kupata report kwa magazeti na vyombo vingine ambavyo mara nyingi tunasikia malalamshi kwamba vinatia chumvi.

Kuhusu Wanyama wa Pori na mbuga, nina mapendekezo haya; Wanyama wa pori wanapoingia na kuharibu mimea, serikali igaramikie fidia za mazao hayo na ikiwa wanyama hawa pengine watakuwa wameingia tu kijijini na hawajafika mashambani-na ni hatari wengine kuwa wanapigiwa report na kama tunavyo ona mara nyingi, huwa hakuna hatua za haraka kuchukuliwa na

inakuwa kwamba hatari inaishi na wenyeji kijijini. Kama muda wa masaa ishirini na nanne itapita kabla serikali kuchukua hatua basi iwe tayari kuhakikisha kwamba imemaanisha kwamba inawatoa wanyama hao kama sadaka kwa wenyeji, kama anaweza kuliwa kama Nyati na Tembo, hiyo mboga ya wananchi. Kama ni simba ambaye hawezi kuliwa, basi atauawa na kama serikali (inaudible).

Kuna kitu ambacho kinaitwa withholding tax. Serikali ninaona imekuwa na rai kidogo kwa sababu pengine mtu ana madai yake ambayo anataka kulipwa, pengine kama mshahara na kwa ajili ya tatizo ambalo huyu muhusika ambaye atalipwa hawezi kujua, ikatokea kwamba serikali haikuweza kumulipa kiasi chote kile kwa pamoja-kimepunguzwa na kile ambacho kimesalia, inakuwa tena kwamba hakipati hicho chote-kuna kila kitu tunaita withholding tax ulikuwa umepanga budget yako, pesa imekuja nusu na hiyo inayobaki uki dai unapewa sio yote; unaambiwa nyingine imekatwa (inaudible).

Wageni wanoapokua wameenda sehemu za watu wengine, ni vizuri wajitambulishe kwa vyombo vya utawala vinavyohusika. Kwanza iwe ni sheria kwamba yule mwenyeji ambaye ametembelewa na mgeni atapiga report kwa mzee wa mtaa ambaye atawakilisha report hiyo kwa mwenzake wa juu na itaenda hivyo-kiasi cha kuweza kuthibitisha usalama kwa kujua mtu huyu ni nani, kutoka wapi, amekuja kwa nani, kwa ajili ya nini, kwa siku ngapi-mambo yawe sawa sawa.

Kuna mambo muhimu ambayo hutangazwa. Serikali inasema kwamba ina Gazeti lake maalum ambalo ndilo inahakikisha kwamba linasema kweli, ambapo tangazo likitoka pale hilo ndilo limethibitishwa kwamba kweli limetoka kwa serikali ni Kenya Gazette. Kama kuta kuwa na kitu ambacho imechapishwa kwa Kenya Gazette, watu ninaamini kwamba kinakuwa ni kitu muhimu sana, mimi sijawai kuona Kenya Gazette-naisikia. Ninafikiri ni vizuri serikali ifikirie kwamba ni sawa wananchi waweze kufikiwa na Kenya Gazette.

Nikimalizia, ni hii Katiba ambayo sasa tunangangana kuirekebisha. Ikiwa ndio uti wa mgongo wa maswala yote-maana imebeba sheria ndani na jinisi ya kutekeleza mambo, nafikiri imefika wakati ambapo pia serikali itabidi iweze kuchapisha vitabu vya sheria na ihakikishe kwamba wananchi wanaweza kuvipata kwa urahisi na kuweza kujisomea ili kujifahamisha kuhusu sheria. Na hii nina amini itaweza kupunguza uvunjaji sheria kwa sababu, watu wengine wanavunja sheria pasipokujua kwamba wanaivunja-na pia itasaidia watu kujitetea-dhidi ya kunyanyaswa kwa sababu mtu mwingine anakosa haki yake kwa sababu ya kutojua sheria inayomlinda. Asante sana.

**Com. Domiziano Ratanya:** Ningetaka kuuliza swali moja hapa. Kenya Gazette unsema wananchi wapewe ama wapatiwe waweze kununua?

**Nimrod Mutangaoru:** Nilikuwa nimekusudia kwamba pengine kama ninakala, inaweza kuja pengine kama ni kwa ma-DO kama kwa ma-Chief ambapo hawa watu wako na wenyeji wataweza kuwaeleza kile ambacho kimetokea (inaudible).

**Com. Domiziano Ratanya:** Tena ningetaka kukujulisha kuwa katika Government Press, hiyo gazetti inauzwa n asioni watu wakinunua.

**Nimrod Mutangaoru**: Sasa kuja kuuzwa (inaudible) kwa sababu unaona kwamba ndio pengine kumnyima haki maana kuna wale wasioweza kununua kama hata hakuwa ameiona na anataka kuinunua ama amesikia, hana uwezo pale (interjection) kwamba ihakikishwe kwamba pengine vyombo ambayo viko karibu na wananchi kama DO's, Chiefs na Assistant Chiefs wapate hizo a waweze kuwambia wananchi wa pale.

**Com. Domiziano Ratanya:** Lakini tena unajua ma-DO wana hizo copies-DC's na ma-DO's.

**Nimrod Matangoru:** Kama ituakuwa (inaudible)lakini (inaudible).

**Com. Domiziano Ratanya:** Kwa hivyo wewe maoni yako unaomba kwamba ziweze kufanyiwa nini ziwe kufika wananchi?(inaudible answer) Pengine hayo ni maoni yako? Kwa hivyo tunashukuru sana Nimrod. Na tuende kwa Gregon K. Nyalo, Gregon hayuko? Julius Matheka? Francis Ndogaine? Councilor Penina? Amepeana memorandum? na hata naona hata Francis alikuwa na memorandum, amepeana huko? Godfrey Jumamosi?

**Godfrey Jumamosi:** Kwa majina yangu ni kama hivyo-Godfrey Jumamosi. Nina maoni machache kuhusu Katiba hii ambayo tunarekebisha hivi sasa, ambayo tumepewa nafasi tutoe maoni yetu. …..ningetaka tu (inaudible) kwamba kuhusu muundo wa serikali ambayo tunaitamani ije kwa wakati huu ambao tunaendea.

Kwa maoni yangu nilikuwa napendelea kwamba tuwe na serikali ya majimbo na majimbo haya yagawanywe kulingana na vile yalivyo hivi sasa-mkoa wa Pwani, kwa mko wa kati na zingenezo na mipaka ya iwe hiyo hiyo. Katika majimbo hayo, nilikuwa na mambo fulani nilikuwa na pendandikeza, na niyaweke wazi kama maoni yangu vile ingeweza kusaidia katika uongozi. Kuanzia chini kabisa pawe na wazee waa mitaa ambao watakuwa wanachaguliwa na wananchi wa sehemu hiyo.

Pili, kuwe na kata ndogo kama zilivyo na hizo kata ziwe pia na Sub-Chief ambaye atakuwa pia anachaguliwa lakini katika uchaguzi ambayo ninapendekeza kuwe kuna kama tume ama njama, kama Wataveta walinyakuwa zamani hapa, walikuwa wana njama kama vile Wakikuyu walivyokuwa na Gema; Basi hao watu wawe ndio watu wanaweza kupendekeza hao watu ambao watatawala hizo kata ndogo maana watakuwa wanawajua na pia watakuwa wana hakikisha kwamba ni watu ambao wanaweza kuongoza watu katika njia inayofa kuliko kuajiriwa straight na serikali. Pili, katika location pawe na Chief ambaye pia atachaguliwa na hao hao watu wa njama ambao watakua wanamujua mtu hule mzuri na katika maongozi yake kama ilivyokuwa hapo zamani.

Pia, katika ngazi za u-division, kuwe na DO ambaye atakuwa ameajiriwa na serikali hiyo ya majimbo na pia napendekeza pawe

na tume maalum ambaye itakuwa anaajiri wale ambao watkuwa wanaanzia katika division. Pia pawe na DC kama ilivyo, lakini awe wamechaguliwa na hiyo hiyo serikali ya majimbo kupitia kwa hiyo tume. Pia pawe na PC ambaye atakuwa ni Governor wa kusimamia jimbo hilo na yeye pia atakuwa ameajiriwa na hiyo tume.

Na vile vile, nilikuwa napendelea kwamba pawe na Bunge la majimbo. Kila jimbo liwe na Bunge lake, ambalo Bunge hilo litakuwa linasimamia maswala yanayohusu jimbo hilo na kutazama maswala yote yanayohusu shida za watu wale. Na hawa Wabunge wawe wanatoka katika zile kabila zinazotoka katika jimbo hilo-kama Wataveta wawe na Mbunge wao, Wataita wawe na Mbunge wao, Wagiriama……….. ata hawa watakuwa na kikao wakijadili maswala yote yanayohusu sehemu zao. Hapo hapo ningelipendelea pia pawe na Bunge la Taifa ambapo wale Wabunge-wakilishi katika majimbo, watakuwa wanachaguliwa wengine kuenda kuwakilisha katika serikali kuu na watakuwa na Rais mmoja ambaye atakuwa pia amechaguliwa kutoka katika majimbo yote na jia ya kumchagua awe amepata asilimia ishirini na tano katika mikoa-inaweza kuwa tano ama sita. Huyo ndiye atakuwa Rais wa Taifa lote ndiye atachukua jukumu la taifa nzima.

Na pia nilikuwa nimeonelea kuwa, kuna maswala yanayohusu mambo kama rasilmali za jimbo. Nilikuwa napendekeza kwamba, kuhusu matatizo kama ardhi, ardhi hii iwe inamilikiwa na wenyeji wa sehemu hiyo-katika hilo jimbo na wageni kama watakuja, wawe ni watu wa kufanya biashara na shuguli zingine. Kama atataka kulima awe anafanya kukondeshwa kwa msimu kama kutokuwa kuna ardhi iliyoko wazi. Na vile vile, matatizo yatakayo kuwa yanatokea, kuziwe kuntengenzwa-labda kama vile kunavyfanyika sasa-kuna watu wanatoka katika wilaya kuja kutatua matatizo ya sehemu zingine na hawajui hali ya matatizo ya ardhi ya mahali pale. Kuwe hawa hawa wazee wa njama ndio wanatatua matatizo, maana wanajua shida ya sehemu lile.

Kuhusu misitu, mara nyingi nimeona misitu mingi imeharibiwa na viongozi wa serikali wale wanaotumwa kwa sehemu ile. Sasa kwa kulinda mali hizi maana chemchemi nyingi za maji inaanzia mistuni, ningependekeza kwamba, pia maswala ya misitu iwe chini ya hizo njama na wawe wakishirikiana na baraza la-yaani Municipal Councils ambazo zitakuwa kwa sehemu hiyo. Pia pawe na Councils ambazo zitakuwa ..madiwani na pia kutakuwa hata na kama ni Town council; hawa watakuwa wanashirikiana na hii njama kwa kuona kwamba maongozi ya sehemu ile yanaenda sawa sawa.

Pia nilikuwa napendekeza kwamba elimu iwekwe wazi kuanzia Standard 1 mpaka 8; Watoto wasomeshwe bure na serikali hiyo ya majimbo. Kwanzia kidato cha kwanza na kuendelea wazazi wagharamie. Vile vile, nilikuwa napendekeza kwamba vyombo vya umma tuseme kama Usalama na mambo mengine, visimamiwe ni serikali kuu ambapo Rais, atakuwa na mamalaka ya kusimamia mambo ya jeshi na mambo mengine ambayo yatahusu usalama katika nchi.

Rasilmali ambazo zitakuwa zinatoka katika sehemu ile ya jimbo-katika sehemu wale watu wanatoka, sehemu ya sabini na tano asilimia iwe inaachiwa watu wa mahali pale na ile ishirini na tano sasa ichukuliwe katika serikali kuu kwa ajili ya matumizi mengine. Vile vile, nilikuwa ninapendekeza kwamba Rais anapokuwa katika hali labda pengine ya kuenda kugombea kiti, muhala wake unapokwisha, basi akabidhi madaraka hayo kwa Speaker. Ni yeye atakuwa na jukumu la kusimamia Serikali-na

afanye handing-over kabla hajaenda kugombenea kiti-kwa Speaker kuhakikisha kwamba mali za umma ziko sawa sawa kabla hajaenda kugombea kiti tena-maana anaweza akashindwa na pia (inaudible)patikana.

Vile vile nilikuwa napendekeza kwamba Rais asiwe ni mtu mtoto awe ni mtu kuanzia umri wa miaka arubaini na kuendelea. Naam, kama amehusika na kashfa ya aina yoyote ile, asiruhisiwe tena kuongoza-kama ufujaji wa mali ya umma, ufisadi na mambo mengine machafu, asiweze kuchaguliwa.

**Com. Domiziano Ratanya:** Okay Bwana Godfrey kama una memorandum unaweza kupeana. Asante sana. Jacob Norman?

**Jacob Norman:** Mimi kwa majina naitwa Jacob Norman nimezaliwa Chale Location. Kwanza, ninaanza kuhusiana na uadhifa wa Rais. Madaraka ambayo Rais ako nayo kama ya kusimamia jeshi yapunguzwe. Pili, Rais awe akikaa katika mamlaka kwa vipindi vitatu vya miaka mitano mitano-vipindi vitatu vya miaka mitano mitano.

Bunge; Katika Bunge ya Kenya, tungeomba wale wanaogombania viti katika Bunge wawe ni wazaliwa wa hiyo sehemu na wawe ni kabila la kutoka hilo sehemu. Hii hi kulinda makabila madogo ili nayo yawakilishiwe katika Bunge la Kenya. Vile vile katika Bunge la Kenya, wakina mama waakilishwe hasa hiki chama cha maendelo ya wakina mama wawakilishwe katika Bunge la Kenya.

Kuhusiana na ma-Chief, ma-Chief wateuliwe na wawe wamezaliwa katika hilo eneo na wawe ni wakaaji wa hiyo sehemu. Upande wa ardhi, ardhi zote ambazo ziko na wageni ambazo zilinyakuliwa wakati wa UKoloni zichukiliwe na serikali, zigawanyiwe wale wananchi wa sehemu hiyo. Kwa mfano, shamba hili ya Ziwani pamoja na la Taveta. Wenyewe warudishiwe mashamba yao.

Swala lingine ambalo ningetaka liwakilishwe katika Katiba hii mpya ambayo tunatengeneza, ni kuhusiana na ulimaji wa mashamba. Tume ihakikishe kumeteuliwa tume ambao itakuwa ikisimamia ugawajie wa mashamba. Na hayo mashamba yagawanyiwe wale wenyeji wa hizo sehemu ikiwa watakuwa na uwezo wakupimiwa hayo mashamba na kupewa title deed.

Kwa upande wa serikali, vile vile tungelitaka tuwe na Waziri Mkuu ambaye atakuwa na mamlaka ya kuteua Baraza la Mawaziri ama kuunda Serikali. Swala lingine ni kuhusu Tume ya uchaguzi. Kuna kipengele ambacho kinatumiwa na Tume ya uchaguzi kwamba kupiga kura mahali popote pale twaomba Katiba igeuze, mtu achukue kura pale mahali amechukulia kitambulisho. Hii nikuwezesha kuzuia ulagai ambao utakuwa unaendelea katika sehemu zingine.

**Com. Domiziano Ratanya:** Okay, asante Norman. Sasa tunaenda kwa huyu mwingine anaitwa Peter Mutua. Peter Mutua yuko karibu?

**Peter Mutua:** Asante sana. Kwa majina mimi ni Peter Mutua na niko hapa kutoa maoni yangu kulingana na Katiba yetu.

Kwanza ninaanza na mambo ya ardhi. Katika nchi yetu ardhi imetumiwa vibaya na kumilikiwa tu na watu wachache wakati watu wengi wanakosa mashamba na kuitwa ma- squatter katika nchi hii. Kwa hivyo mapendekezo yangu yangekuwa ni kwamba ardhi iwe ni mali ya taifa na itumiwe kwa ajili ya watu wote wa nchi hii. Kila mtu akipata fungu sawa, na kuitumia tu sehemu anayoweza kutumia na ile ingine, asimilki shamba haina kazi. Kwa hivyo ni mali ya taifa kwa watu wote.

Ya pili, nazungumzia juu ya mali asili. Nchi yetu ina mali nyingi sana ya asili kama maji ambayo yankitumiwa vizuri, watu wata irrigate nchi nzima na kutoa mazao na mali ya kutosha. Kwa hivyo, mali ya asili kama maji yatumiwe (inaudible) wote kwa nchi na wananchi wasaidike na hayo maji kwa irrigation na kunywa maji masafi ili waweze (inaudible) nzuri. Pia kuna mali zingine za asili kama matumishi ya jua, kama solar energy, ambayo inaweza kutumika kwa kupunguza garama ya mahitaji ya maisha ya watu ya nyumbani na kutengeneza mahitaji ya kuleta moto-vitu vya kutumia nyumbani kama kupikia na watu wakapunguziwe gharama za matumishi yao ya (inaudible) ama ya vitu kama hizo.

Pia kuna mali zingine za asili kama madini. Ningependelea madini yatumike kwa nchi lakini sehemu yanayotoka, watu wapatiwe percentage fulani wakibaki nayo, kwa sababu ni sehemu hiyo hiyo mali inapatikana. Kwa mfano, wapate hamsini kwa mia ya ile mali inatoka pale- wale wenyeji wa sehemu madini imetoka na mali zingine kama hizo.

Sehemu ninayoelekea ni ya elimu-education; ningeomba elimu iwe ya bure kuanzia nursery mpaka darasa ya nane lakini siyo bure ambayo tunasema kuna kugawana garama. Iwe ni bure kabisa watoto wasome bila kuangaika. Sehemu ingine ningezungumzia ni kuhusu mambo ya kazi-ukosefu ya kazi. Ningeomba watu wote ambao wamemaliza kusoma na hawana kazi serikali iwalipe kiwango fulani ya kuhudhumia maisha yao ili wasije wakawa wezi na kuharibu nchi yetu kwa kuibia watu wengine; Lakini walipwe mapato fulani ya nchi ili wajiweke katika maisha kama watu wengine wakikojea wakati ule kazi itatokea. Na kwa hivyo hawatajiunga na genge za wizi na kutumia mabavu kunyanganya wengine.

Jambo lingine ningezungumzia ni kuhusu makabila ya Kenya. Katika nchi yetu bado ukabila unaonekana unaenda hali ya juu sana na utaifa unafifia. Kwa hivyo ningeomba hali ya kuhusika ukabila wa Kenya, watu waendelee kuinuliwa kuwa taifa moja na makabila ikiwezekana, yanze kufifia na kupotea. Kwa mfano makabila kwa majina yasiwe yanajulikana sana, lakini labda ikiwezekana, kuwe na number za makabila tu kujua hii ni community fulani-lakini kusiwe na makabila ya kutambulisha watu kwa misingi ya kikabila- lakini utaifa uchukue nafasi ya kwanza.

Ninazungumzia tena haki za watu. Haki za watu ninangalia upande wa wanawake, katika haki za watu, wanawake wamenyanyawa kwa mambo mengi. Kwa mfano, tunaona siku hizi wanawake wanatumiwa kama vyombo tu vya kuzaa watoto na mara akizaa anaweza kutupwa na bwana na akaachwa na labda bwana akamilikia wale watoto kama mali yake na

kumufukuza mama. Ningeuliza Katiba isimamie wanawake kwamba, mtu yoyote akikaa na mwanamke, awe ni lazima amuweke kama bibi yake hata kama kunatokea shida gani, kwa sababu amemuharibia maisha na hawezi kumutupa. Tunaona pia wengine wawatung mimba washichana akizaa naye watoto wawili, anamutupa pamoja na watoto na hawa watoto ndio wanaenda kuwa street children-ama watoto wanaozurura mtaani. Hali hiyo pia ingewekwa kwa yoyote anayezaa na msichana alazimishwe kukaa naye kama bibi yake bila kumuwacha kwa vyovyote, ili kusitokee watoto wanazurura mitaani na wanawake waliochanganyikiwa kwende kufanya mambo ya umalaya bila kufuata maisha ya kujiudumia.

Hali ingine ningeangalia ni hii unyanyasaji wa watoto kufanya kazi kwa sababu ya shida. Itolewe sheria kali ili watoto wadogo wasifanye kwa vyovyote kazi ya kuandikwa-kuajiliwa; la hivyo, mtu yoyote akipatikana apadhibiwe ili watoto wapate haki yao ya kusoma.

Upande mwingine ni hali ya kunyanyasa ile gender ya akina mama kama wanawake kwa kunajisi ubakaji na vitu kama hizo. Mambo hayo yangechukuliwa kwa hali ya juu sana na kutolewa hukumu ya juu, ili wanawake wapate uhuru kwa kuwa na haki katika maisha yao. Lingine ningezungumzia ni upande wa dini. Kutolewe sheria kwamba sio kila mtu anayetaka kuandikisha dini bila kujulikana ni ya aina gani, anaruhusiwa na anapewa kibali. Lakini dini ziwe na mikataba. Kusitokee dini kama vile unaona uabudu wa shetani unaendelea katika nchi hii na ni watu ambao wamejiandikisha kisheria na wanajulikana. Wengine wanafungua hatamakanisa unakuta ni waabundu wa shetani. Kwa hivyo hali hiyo ithibithishwe kwamba dini ijulikane ni aina gani na inafunza mielekeo gani ya imani na kama ni mibaya iweze kuzuiwa. Kwa hivyo kusiwe na haki tu ya kuabudu bila kuwa na mipaka(interjection) Kidogo nilikuwa na mengine machache.

Nilikuwa nasungumzia kuhusu uchaguzi wa Rais. Rais angekuwa mtu asiye jiunga na chama chochote, awe mtu independent na asiwe juu ya sheria. Awe Rais anaweza kushtakiwa kama mikosa akiwa kazini. Lingine ambalo ningezungmizia ni Members wa Parliament. Katiba ingelinda wananchi kama yoyote aliyechaguliwa kama Member wa Parliament hawatumikii vizuri, aondelewe na wachague mwingine ili aweze kuwatumikia.

Kwa upande wa vyama vya kisiasa, maoni yangu ni kwamba tungekuwa tu na vyama viwili vya kisiasa-yaani kinachotawala ni cha upisani kimoja. Na serikali ikivunjwa, Speaker aweze kushikilia mpaka itakapochaguliwa nyingine. Jambo lingine ningeomba uchumi wa nchi ugawanywe sawa kwa nchi nzima kulingana vile watu wanatoa kodi ili mali ya nchi igawe sawa kwa watu wote.

Security; ningeomba wananchi waruhusiwe kumiliki silaha ya kujilinda kama bunduki kwa sababu security ya nchi hii imekuwa hatari, watu wanauwawa ovyo na kwa hivyo wakiwa na shilaha pia watajikinga na watajua namna ya kujikinga na ujambazi wanao wasjambulia. Asante sana.

**Com. Domiziano Ratanya:** Okay, asante sana Peter Mutua kwa hayo mengi-ulisema ni machache lakini ni mengi kidogo na

ni mazuri lakini nikiangalia, tunaende kumaliza na huyu anitwa Josephat Ritimiru. Josephat yuko?

**Josephat Ritimiru:** Majina yangu ni hayo mumeyasikia Josephat Ritimiru, mimi ni mkaaji wa hapa Taveta, Chale. Kwa maoni yangu-mimi sina kisomo (inaudible) mimi ni Mukulima lakini hinavyona wanyama wa kutoka Porini waningia ndani ya shamba (inaudible) hata watoto wangu hata shule wanashindwa kuenda kwa sababu ya njaa. Hilo jambo kwa kweli wazazi tun kilio kikubwa. Basi tungeomba ikiwezekana kabisa, serikali ambao itakayo kuja ijaribu kutunza wanyama hawa wasilngilie dani ya mashamba za watu. Hawa wanyama zamani wakati wa ukoloni walikuwa, wakila namna hizo na ilikuwa inarudisha nguvu-kwa sababu kukiwa huna chakula unatafuna nyama na watoto wanalala-siku hizi hairusiwi. Tuna madai mengi tuna dai mashamba, ………hayajalipwa mpaka wa leo hii kwa hivyo huo ni unyanyasaji kwa upande wa wakulima.

La pili, narudi hapa kwa upande wa ufugaji. Ufuzaji mifugo tunashindwa kuona sehemu za kukula na mifugo wameanza kuwa wachache hapa Taveta kwa sababu sehemu zilizotengwa za kuchunga-kufugia nyuki, zote zimeshapata wananchi wameingia na hata kama ni watu wa Kenya-MKenya ni MKenya wakati ameingiea mahali kihalali.(inaudible) Nauziwa shamba nimetoka sehemu nyingine huko, ninaishi hapo kama mwenyeji kwa sababu hii ardhi ni ya halali, nimeinunua. Lakini kama utaingia mbuga za wanyama zilizotengwa na ukiambiwa "bwana hapa mahali pa kuishi hapa ni pangea" unasema mimi ni MKenya utanipeleka wapi? na unazidi kuendelea na kuishi. Na wakati unampeleka kwa sheria, unakuta ile sheria milango zote zimefungwa. Kwa hivyo tunazidi kuendelea na kupambana miaka na huko bado mambo hatuelewani dani ya ile sehemu. Napendekeza ya kwamba, kweli sisi tu wananchi wa Kenya na popote tunaweza kuishi, lakini kama nikija kwako nikingia mahali umevamia, nikilalamika ni sikizwe-na sheria iangalie kwamba nani mkosefu pale ili tuweze kudhumishwa undugu. Tuweze kugawanyiwa. Kama si hivyo mimi sina haki niondoke-ama yule ana haki apate haki ili tuweze kuishi usalama. (inaudible) imejaa (inaudible) hapa Taveta na kwa sababu malalamizini mengi sana hapa.

Ile jambo ni kwamba sheria itengwe na iwekwe wazi kwamba wataangalie haki. Wale ambao hawana mali mengi wanakufa (inaudible) gharama zimepanda ndani ya mahospitali Kiasi cha kwamba unaweza kuangalia hata mtoto akikufa kwa sababu hauna uwezo. Serikali iangalie hapo. Serikaliile ambayo itatawala, tafadhali iongahe mahali hapo. Napedekeza hizo gharama zipunguzwe na pawe pana mtu ambaye anaweza kutembelea mahospitali kupea hizo dawa serikali iwa inaleta zinaenda wapi?

Ya pili, shule kama hivi sasa tunasikia watoto wanasoma (inaudible) kusoma bure; Kama ni kweli, iendelee hivyo maana wazazi wengi hawana uwezo wa kusomesha watoto. Pia gharama ni kubwa. Pendekezo; waruhusiwe kusoma bure (inaudible) zile ambazo zitaonekana kwamba ni (inaudible) kwa wazazi na kuhakikisha watoto wanaenda bila wazazi kusumbuliwa. (inaudible) Pia naye aangaliwe maana gharama ukiweka juu zaidi yule ana mtoto wake hatasoma. Kwa hivyo, ningeomba kwamba tuangaliwe upande wa masomo. Ya pili, kutiwe wazi kwamba kuna njia ya kupita-tuandikishe uelewano.. Unajua mtu kama mimi na wewe tunayonganyana, mimi ninakunyanganya (inaudible) tupatiwe njia ya kuangaliwa sheria iwekwe wazi-----

Halafu ya pili, ni hii kitu kinaitwa Bunge. Bunge, ukiangalia kila nchi mwananchi wa nchi hiyo ndiye Mbunge nidye

mutawala(inaudible) Tunaomba, kuwekwe wazi sisi kuwe na nafasi kujitawala (inaudible)-- anatoka huko kuja kutusimamia hapa---- Nimemaliza.

**Com. Domiziano Ratanya:** Kuna yeyote amejiadikisha na haja-peana maoni yake? Imeisha? Mumekubali mumeisha? Asante sana.(inaudible) Pastor hebu utubarikie hayo yote tume fanya leo.

**Pastor: (Prayers):** Haya, simama tumalize kwa maombi.

Baba katika jina la Yesu hatuna budi kukushukuru kwa ajili ya siku ya jana na pia ya leo; jinsi umeendelea kuwa mwaminifu, ukaendelea kupatia ma-Commissioner wetu nguvu, Secretary pamoja na Programming Officer, asante kwa ajili ya uwepowako na ushindi wako. Sasa watumishi wako wanarudi nyumbani, Mungu uendelee kuandamana nao wanaporudi nyumbani, na ma-Commissioner wetu wanapo safiri kuenda sehemu za Mombasa, ukaendelee kuwabariki na pia ukasimame nao kwa jukumu kubwa ulio wapa Bwana la kurekebisha Katiba hii yetu ya Kenya. Asante Bwana kwa uwepo wako na ni katika jina lako Baba tunaomba haya na kuamini, Amen.

The hearing ended at 3.30 p.m.

**&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&**